

EE BWANA, MARA MOJA TU ZAIDI



Habari za asubuhi, marafiki, ama habari za alasiri. Nilivunja saa yangu ya mkono, sijui ni saa ngapi. [Ndugu mmoja anasema, “Ingali ni asubuhi, ndugu.”—Mh.] Ingali ni asubuhi, ndivyo? Vema.

² Licha ya hayo, tunaishi katika Umilele. Hatuna wakati. Vikomo vya wakati vilikoma wakati Yesu Kristo aliponipa Uzima Wake ndani yangu, niishi kwa huo, kwa hiyo sisi ni viumbe vya Milele sasa hivi, tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu. Ni wakati wa jinsi gani!

³ Sasa hii ni siku yangu ya pili tu hapa pamoja nanyi, lakini, jamani, ni kama sukari ya rojorojo baridi asubuhi, ni nzito sana na ya ajabu. Sijapata kujifurahisha zaidi katika mkutano wowote. Nami ninaangalia huku sasa usiku, wamesongamana sana siwezi kuona mtu yeyote, bali leo hii ninaweza kuangalia kote. Nilikuwa na majaliwa ya kupeana mikono na hili kundi zuri la wahudumu katika kundi hili hapa.

⁴ Ninakumbuka mzee mmoja aliyekuwa akija kanisani mwetu, jina lake John Ryan. Mzee Ryan, walimwita. Alitoka Dowagiac, Michigan. Naye alikuwa akihubiri kidogo, kisha anakimbia nyuma na kunipa mkono. Kisha angehubiri kidogo, na kurudi mbio na kunipa mkono. Nikasema, “Ndugu Ryan, ni—ninathamini hilo, bali si—sielewi maana ya wewe kufanya hivyo.”

⁵ Akasema, “Wakati betri inapopungua moto, ninahitaji kuichaji, kwa hiyo nimetiwa chaji kabisa.”

⁶ Ndio kwanza nimwone m—mhudumu wa Kimethodisti kutoka huko juu nchini mwangu, ambaye ndiyo kwanza ampokee Roho Mtakatifu, nami nilimbatiza. Anayeketi hapa mkono wangu wa kushoto, Ndugu Junior Jackson. Nilimwona akitikisa mikono yake namna hiyo, kidogo ilinikumbusha juu ya Ndugu Ryan. Ni wangapi wanafikiri ya kwamba Wamethodisti hawawezi kumpokea Roho Mtakatifu? Mmekosea. Simama, Ndugu Junior Jackson, yeye na mke wake mpendwa pale. Wametoka huko chini Indiana, mhudumu Mmethodisti.

⁷ Yuko wapi Willard Collins? Yuko jengoni asubuhi ya leo? Uko wapi, Ndugu Willard? Nilidhani alikuwa hapa karibu. Mhudumu mwingine wa Kimethodisti aliyesimama hapa, kama hufikirii Wamethodisti wanaweza kumpokea Roho Mtakatifu na kubatizwa tena. Simama, Ndugu Collins. Huyu hapo mwingine. Huyu ndugu alikuwa huko kwenye Chuo cha Asbury huko Wilmore, Kentucky, kutoka kwenye msingi mzuri wa Kimethodisti.

8 Sasa wapo watu wengine wengi pamoja nami hapa, ambao—ambao wameshuka kuja huku. Niliwasikia wakisema “amina,” nami najua wapo hapa, bali siwezi kuwaona. Ndugu—Ndugu Fred Sothmann kutoka kwenye maskani huko Jeffersonville. Fred, wewe na Ndugu Tom mpo hapa? Ninaamini ninamsikia akisema, “Hapa.” Hapa pembeni, naam.

9 Tuna furaha sana kuwatambulisha watu hawa. Sioni vizuri hasa kwenye wakati huu, labda kuna wengine zaidi hapa ambao siwajui. Nafikiri Ndugu Jack Moore ndio kwanza amalize kuzungumza. Na—na kwa hiyo hawa ni watu wazuri, nasi tunawapenda.

10 Na sasa umekuwa ni wakati mzuri sana wa kuwa hapa. Nilimwambia mke wetu, mke wangu, nikasema, “Laiti, laiti ungalishuka uje kwenye mkutano huu.” Tunaamini katika mkutano mzuri wa kipentekoste wa mtindo wa kale. Tunaamini, ya kwamba palipo na uhuru katika Roho wa Mungu, kwamba sura zote mbalimbali za madhehebu zinaweza kukutanika pamoja na kuketi pamoja katika ulimwengu wa Roho, kama kanisa. Tofauti zetu hazileti tofauti yoyote kule, tunapokuwa ndani ya Kristo, tuko chini ya Damu na katika ushirika wa upendo Wake.

11 Nami ninataka kusema jambo hili kwa kundi hili la wahudumu. Ni—nilingia katika Pentekoste kutoka kwenye Baptisti ya Kimishenari, nami nimevutiwa na Pentekoste. Hao ni watu wangu. Ninawapenda. Kama niliwazia kulikuwako na kanisa lolote lililo sahihi kuliko hilo, ningekuwa kwenye kanisa hilo lingine. Bali niko pamoja na Wapentekoste, kwa sababu ninafikiri ndicho kitu kilicho karibu sana na Maandiko ninachokiona. Kama ningalijua kitu kingine, ningekuwa pamoja nao; na kwa hiyo, sio kupuuza imani nyingine yoyote, hata kidogo. Lakini sababu ya mimi kuiwazia Pentekoste, kwa sababu iko karibu na kile ninachowazia ni cha Kimaandiko, kuliko chochote nijuacho.

12 Na kuna jambo moja zuri sana katika mkutano huu, ambalo nimeliona, hilo ni, wanawake wenye nyuso safi; hakuna hiyo rangi ya makucha, mwajua, ama vyovyote mnavyoviita vikorokoro hivyo. Sipendi hilo. Hilo haliwafai Wakristo. Ha-ha. Hiyo ni kweli. Na—napenda hilo. Mimi ni mfuasi wa mtindo wa kale unaopenda usafi, mnaona. Ninapenda kuona wanawake... Mnajua, simaanishi...

13 Hapa si mahali pa kusema lolote, mizaha na kukufuru, kusema hivyo. Lakini sisemi hili kwa maana hiyo. Hapa si mahali pa hilo.

14 Jambo lingine, ninyi nyote mlipata kitu hiki lini? Hiki kinatoka kwenye maskani yangu, inaonekana. Hakika kinatoka kule. Hiyo ni kweli, kanisa? Hiyo si inaonekana kama ile

mimbara ya zamani? Vema, nafikiri maskini Ujumbe ule ule wa kale tunaohubiri kule unasambaa kote, kwa vyovyote vile.

¹⁵ Kwa hiyo mnajua, kuna mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyepata kujipaka rangi usoni. Naye kamwe hakujipaka rangi usoni ili kukutana na Mungu. Alipaka uso wake rangi ili kukutana na mwanamume. Hiyo ni kweli. Mnajua kile Mungu alichomfanyia? Alimtumia kuwalisha mbwa. Kwa hiyo unapomwona mwanamke amejipaka rangi, wewe sema tu, “Habari za asubuhi, Bi Nyama ya Mbwa.” Hivyo ndivyo ilivyo hasa. Hilo ni la kuchukiza sana, sivyo? Lakini hivyo ndivyo Mungu anavyoliwazia. Amefanywa tu chakula cha kawaida cha mbwa kwa ajili ya mbwa mwitu. Hivyo karibu ndivyo alivyo. Baadhi ya hawa mbwa mwitu washenzi wanaotangatanga, wikipiga mbinja, mwajua; kile wanachokiita mluzi ashiki, mwajua. Hivyo ndivyo ilivyo, nyama ya mbwa tu tena.

¹⁶ Nina shukrani kwa ajili yenu enyi wanawake. Mungu ajalie neema kuwashikilia mbele ya msalaba, myaondokee mambo haya ya duniani. Hata hivyo, tuko njiani mwetu kuelekea Utukufuni. Sisi ni wenyeji wa Ufalme mwingine.

¹⁷ Muda mrefu uliopita . . . nilikuwa tu nikiangalia kote kwenye kusanyiko nione kama ningeweza kumwona mmoja wa hao watu, na hao ni baadhi ya marafiki zetu weusi, Wanegro. Mwajua, muda mrefu uliopita, hapa chini Kusini, walikuwa wakiwafanya watumwa. Sasa, mimi ni Mkusini. Na kuna jambo moja ningetaka kusema juu yao, laiti ningaliweza kuzungumza na Martin Luther King. Mtu huyo, akiwa ni Mkristo, hajui anawaongoza watu wake moja kwa moja kuingia katika mtego wa mauti, ambako kutakuwa na mamilioni wao watakaouawa. Mnaona? Amekosea.

¹⁸ Ninawapenda ndugu zangu, ndugu zangu weusi. Nisingekuwa huko Afrika na kote, nikiwahubiria, kama sikuwapenda. Hao ni watu wa Mungu, sawa na tulivyo sisi. Lakini siamini ya kwamba . . . Mtu huyo, chini ya hili, atasababisha tu wengi, wengi wao zaidi kuuawa. Ndipo itaanzisha mapinduzi tena, ambayo kamwe haitaondokea watu hapa chini. Kwa hiyo hao si watumwa. Wana uhuru mwingi kama mtu yeyote mwingine. Hao, kama walikuwa ni watumwa, ningekuwa upande huo. Lakini hao si watumwa.

¹⁹ Ni kwa sababu tu wanataka kwenda shuleni. Wanazo shule. Acheni waende shuleni. Hiyo ni kweli.

²⁰ Alikuwa pale, kumbukeni maskini yule ndugu mweusi aliyesimama pale, asubuhi ile, kwenye ghasia hizo. Aliwaomba wanamgambo kama angeweza kuzungumza. Akasema, “Kamwe sijaone aibu kuwa mtu mweusi. Muumba wangu alinifanya mtu mweusi. Lakini asubuhi ya leo, ninaona aibu jinsi jamii yangu inavyotenda. Hao watu wanatufanyia kitu gani? Wamekuwa tu wema kwetu.”

21 “Mwanamke mzungu,” alisimama na kusema, “Sitaki watoto wangu wafundishwe na mwanamke mzungu,” kasema, “kwa sababu wao. . . hatakuwa na sha—shauku, kushughulikia watoto wangu kama mwanamke mweusi alivyokuwa katika jamii yangu mwenyewe.” Kasema, “Hapo, hebu angalieni shule zetu. Zina vidimbwi vya kuogelea. Wana shule nzuri zaidi na kila kitu. Kwa nini tunataka kwenda kwenye shule zao?” Hiyo ni kweli.

22 Ninaamini Mungu ni Mungu wa—wa, vema, ningesema Yeye ni Mungu wa vitu vya namna nyingi. Yeye hufanya milima mikubwa na milima midogo. Hufanya majangwa. Hufanya misitu. Humfanya mzungu, mtu mweusi, mtu mwekundu. Hatupaswi kamwe kuwachanganya hao. Inakuwa chotara. Na chochote chotara hakiwezi kujizaa chenyewe tena. Unaiangamiza jamii ya watu. Kuna mambo fulani kuhusu mtu mweusi ambayo mzungu hata hana hizo sifa. Mzungu daima ana kiherehere na mahangaiko; mtu mweusi ameridhika na hali aliyomo, kwa hiyo hawahitaji mambo hayo.

23 Lakini huko nyuma kwenye wakati wa watumwa, walikuwa wakiwauza watumwa, wanadamu, kama kupiga mnada, jinsi wangelifanya gari la mtumba. Kulikuwako na mnunuzi aliyejitokeza, kupitia nchini, naye angewanunua, kisha anaenda kuwauza na kupata faida yake, kama vile ungefanya na gari la mtumba ama chochote kile.

24 Kamwe haikuwa mpango wa Mungu! Mungu alimuumba mwanadamu; mwanadamu akawafanya watumwa. Mmoja hapaswi kumtawala mwingine. Tunapaswa kuishi pamoja katika umoja na amani.

25 Ndipo mtu huyu akaja kwenye shamba kubwa la kale. A—anataka. “Una watumwa wangapi?”

Kasema, “Mia moja ama zaidi.”

26 Alikuwa akiwakagua, na ikatokea kwamba aliona, kulikuwako na mtumwa mmoja miongoni mwa watu hao. . .

27 Hao watumwa walikuwa na huzuni. Makaburu wa Afrika walikuwa wamewakamata hao watumwa, wakawaleta huku na kufanya, na kuwauza. Nao walijua kamwe wasingeweza kurudi kwenye nchi ya wenyeji wao. Walijua walikuwa hapa maishani mwao mwote. Wasingeweza kuwaona watoto wao tena. Kamwe hawatawaona baba na mama. Walikuwa hapa kwa wakati wote, nao walikuwa na huzuni. Na hata wangebeba mijeledi, na kuwacharaza, kuwafanya wafanye kazi. Na kwa hiyo ilibidi kuwafanya wafanye kazi, kwa sababu hawakutaka kufanya kazi. Wote walikuwa wamevurugika kabisa.

28 Huyu mnunuzi wa watumwa akaangalia kule. Ndipo akaona miongoni mwa watumwa hawa, kulikuwako na jamaa mmoja kijana. Haikuwabidi kumcharaza; kifua mbele, kidevu juu, moja

kwa moja kazini. Ndipo huyo dalali akamwambia mwenye hao watumwa, kasema, “Ninataka kumnunua yule mtumwa.”

Kasema, “Hauzwi.”

Akasema, “Anaonekana kuwa tofauti na watumwa wengine.”

Akasema, “Ni tofauti.”

²⁹ Kasema, “Nini kinacholeta tofauti? Yeye ni boshi wa hao wengine?”

Akasema, “La, la. Yeye ni mtumwa tu.”

³⁰ Kasema, “Labda unamlisha tofauti na unavyowalisha hao wengine.”

³¹ Akasema, “La, yeye hula manchani pamoja na watumwa wengine.”

Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana hivi?”

³² Kasema, “Daima nilishangazwa na hilo, mimi mwenyewe, mpaka nilipogundua. Huko kwenye nchi ya wenyeji wao, huko Afrika alikotoka, baba yake ni mfalme wa kabila. Na haidhuru yuko wapi, angali anajua yeye ni mwana wa mfalme, na anatenda kama mmoja.”

³³ Haleluya! Kama wewe ni binti wa Mfalme, basi usitende kama ulimwengu. Kama wewe ni mwana wa Mfalme, usitende kama ulimwengu. Sisi, tunajua ya kwamba sisi ni wana na binti za Mungu. Ingawa tuko hapa katika ulimwengu wenye giza wa mauti na huzuni, hata hivyo tunajua mahali urithi wetu ulipo. Sisi ni wana na binti za Mfalme; sio mfalme fulani, bali yule Mfalme. Hebu na tutende hivyo.

³⁴ Dakika chache zilizopita, sababu ya mimi kuchelewa, maskini msichana Mwethiopia aliyekuwa akiandaa chumba, nami niliona alikuwa akifanya jambo fulani. Nilikuwa nikijaribu kuandika Maandiko fulani kwa ajili ya jambo fulani nililotaka kuzungumzia. Siji kuzungumza ili tu nipate kusikilizwa; naja kusema jambo fulani litakalolisaidia kanisa, kutoa msada kidogo. Na ndipo nilikuwa nikisoma, naye maskini msichana huyu kidogo aliendelea kusita-sita huku. Moja kwa moja akasema, “Utaniwia radhi, bwana?”

Nami nikasema, “Naam, mama.”

³⁵ Naye akasema, “Wananiambia wewe ndiye mtu ambaye aliyepata kibali mbele za Mungu, ya kwamba unapowaombea wagonjwa, kwamba Mungu huyajibu maombi yako.”

³⁶ Nikasema, “Yeye hajibu yangu pekee, bali humjibu yeyote ambaye atamwamini Yeye.”

³⁷ Akasema, “Mimi ni mgonjwa, bwana. Lingekuwa ni jambo lisilo sawa kama nikikuomba uniombe dua kidogo?”

Nikasema, “Sivyo hasha.”

³⁸ Nikamwendea. Nikaomba kitu kama hiki. “Bwana Yesu, miaka mingi iliyopita, ulipokuwa ukiuburura msalaba wa kale unaoparua ukipanda kilima chenye mchanga, na ukiziburura alama za miguu ya Damu iliyokuwa ikichiririka kutoka mgongoni Mwako. Maskini mwili Wako mnyonge, ulidhoofika sana hata Wewe ukaanguka chini ya mzigo huo. Kulikuwako mtu aliyesimama hapo karibu, jina lake Simoni, Mnegro, aliuchukua huo msalaba na akakusaidia Wewe kuubeba. Huyu hapa mmoja wa watoto wake, asubuhi ya leo, mgonjwa.” Yapata wakati huo, likatukia. Mnaona? Yeye ni Mungu wa jamii yote ya mwanadamu.

³⁹ Sasa, marafiki, ninyi ni kusanyiko zuri sana. Nami nikiwa nimekuja kutoka hudumani, ya misheni huko ng’ambo, mbele ya pepo na wachawi, na kadhalika. Kamwe usifikiri hawatakupa changamoto. Inakupasa kujua kile unachozungumzia unapokuja mbele zao. Lakini chini ya kitu kama hicho, halafu kuja huku ambako mioto ya nyumbani inawaka miongoni mwa Wakristo, na kadhalika, hujui ni kufunguliwa kwa jinsi gani kwa mtu kusimama namna hii. Laiti ningaliketi tu kitako pale kwenye kusanyiko na kuwasikia hawa ndugu wazuri waliopakwa mafuta wakilibiri Neno, nami ningeinua tu mikono yangu na kulia, na kupaza sauti, na kuomba. Basi ni—ni—ni jambo la namna gani, kuota huo Moto. Ni jambo zuri sana. Ila kwa kawaida . . .

⁴⁰ Ndugu zangu, nina ndugu wengi sana wanaonipenda, nao wananiomba nizungumze. Na kwa hiyo ninajua, kwamba kuitwa kwenye huduma ya Mfalme, lazima nijaribu kufanya kazi vizuri niwezavyo, bali sikuzote ninaifanya kupita kiasi kwa kukaa kwa muda mrefu kupita kiasi. Nami ninajua ya kwamba mnakingojea chakula chenu cha jioni, mmekuwa hapa tangu saa mbili asubuhi ya leo, ama kitu fulani, katika kundi hili la watu. Lakini niliwazia ya kwamba, kuja alasiri ya leo kuwazungumzia kwa muda kidogo tu, niliandika muhtasari fulani hapa, na Maandiko fulani, ambayo ningetaka kuyarejea. Na katika kufanya jambo hili, nikiwazia ya kwamba mna watu hapa ambao wanastahili zaidi, na wito wa Mungu, kupachukua mahali hapa, kuliko mimi. Lakini langu ni maombi kwa ajili ya wagonjwa, kuona maono, na kadhalika.

⁴¹ Nami nilikuwa nikizungumza na mtu fulani dakika chache zilizopita. Ukiangalia kwenye gazeti la *Life*, mwezi uliopita, utaona hapo. Nanyi mna kanda hiyo. Mimi si mwuza kanda. Lakini kama ulipata kuamini Maneno ninayohubiri, na unaweza kuimudu, chukua *Ile Mihuri Saba*, na kwanza chukua *Ni Wakati Gani, Mabwana?* Sikiliza yale yaliyozungumziwa, miezi sita kabla hayajatukia. Na sayansi imeduwaa. Nikisimama moja kwa moja chini ya pale lilipokuwa likitukia kule. Na kuwaambia, miezi sita kabla, jinsi ambavyo kungekuwako na Malaika saba katika umbo la kundi la nyota, na litaonekana kama piramidi, wangeshuka chini. Na mimi nitakuwa nimesimama

kaskazini mwa Tucson, Arizona, na kutakuwako na mngurumo ambao hata ungeyatikisa mawe kutoka milimani. Ndugu Fred Sothmann anayeketi pale, ambaye alikuwa amesimama pamoja nasi, wengi wao, wakati lilipotukia.

⁴² Sasa sayansi ilipiga picha Yake, mliiona Hiyo, ikaingia kwenye Associated Press. Hawakujua Hiyo ilikuwa ni kitu gani. Hilo hapo Wingu likining'inia, maili ishirini na sita kwenda juu. Hiyo ni maili kumi na tano, ama ishirini, juu hata ya mahali unyevu ulipo. Hawajui kwamba hiyo inahusu nini, nao wanajaribu kuichunguza Hiyo. Na pale, moja kwa moja chini Yake, nilikuwa nimesimama. Nao hao Malaika saba wakinguruma kwa sauti zao, za hiyo Mihuri Saba, wakisimama pale. Na shahidi, sisi watatu, kama shahidi wa mambo yaliyotabiriwa kwenye kanda, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Na pale sasa wanajaribu kuchunguza. Ni siri kwao.

Baadhi yao walisema, “Nenda, nenda, kwa nini usiende ukawaambie?”

⁴³ Ingekuwa ni kama tu wakati Malaika wa Bwana alipojitokeza hapa Houston, Texas, katika ile Nuru. Niliwaambia watu, “Maishani mwangu mwote nimeiona hiyo Nuru.”

⁴⁴ Kanisa linajua hilo. Sayansi inalijua. Ni, kila kitu hakina budi kushuhudia wakati Yesu Kristo anapotenda kazi. Hiyo hapo. Lile jarida, kama ukitaka kuangalia ndani yake, ni lile lililo na Rockefeller na mke wake mpya upande wa nyuma. Nafikiri ni toleo la Mei la jarida la *Life*. Yeye ni Mungu. Tunaishi katika siku za mwisho.

⁴⁵ Sasa nimekuja asubuhi ya leo kujaribu kuchukua muhtasari kidogo hapa, na kadhalika, kuzungumzia jambo fulani ambalo lingelisaidia kanisa, lingesaidia pamoja na hawa ndugu wahudumu, kufanya kazi kwa bidii pamoja na watu hawa. Sisi ni ndugu, nao wananileta hapa kwa sababu wanaamini katika huduma ile ile. Umeokoka katika mkutano huu, kwa nini usichukue ushiriki wako pamoja na baadhi ya haya makanisa mazuri hapa ambayo yanaamini katika huduma ya namna hii. Wao, wanaamini, wanasimama nyuma yake. Na mimi—mimi naja ili tupate kuyaweka chini Maandiko na kwa ajili ya jambo fulani linaloweza kulisaidia kanisa.

⁴⁶ Na somo langu, kama vile, asubuhi ya leo, ni kwenye hali ambayo nafikiri kanisa la Kipentekoste liko la siku hii. Ni msimamo gani na ni wakati upi tumesimama, na uwezekano ni upi? Sasa hebu ninukuu hilo tena. Hali ambamo kanisa limesimama sasa, na uwezekano upi ulioko mbele kwa ajili yake?

⁴⁷ Ninataka kusoma kutoka kwenye Maandiko, kwa ajili ya somo, nami nataka kusoma kutoka kwenye Kitabu cha Waamuzi, mlango wa 16, vifungu vya 27 na 28.

Basi nyumba ile ilikuwa imejaa watu waume kwa wake; na wakuu wote wa Wafilisti walikuwamo humo, na juu ya dari palikuwa na watu elfu tatu waume kwa wake, na wakatazama wakati Samsoni alipocheza.

Samsoni akamwita BWANA, akasema, Ee Bwana MUNGU, unikumbuke, nakuomba, . . . ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu, Ee BWANA, ili nipate . . . kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili.

⁴⁸ Ningetaka kutoa somo kutoka kwenye hilo, kutokana na hayo *Ee Bwana, Mara Moja Tu Zaidi*. Bwana na abariki kusomwa kwa Neno Lake.

⁴⁹ Hapana budi ilikuwa ni a—alasiri ya kupendeza, kitu kama tunachokifurahia leo hii hapa kwenye uwanja huu wa mikutano, hapa Hot Springs, Arkansas. Basi kulikuwa na sherehe kubwa iliyokuwa ikiendelea, lakini kinyume sana na sherehe ilivyo leo hii. Kulikuwako na yapata Wafilisti elfu tatu wakiangalia chini kutoka kwenye dari, watu wawili wa kipekee walioingia kwenye uwanja huo mkubwa wa michezo, na majemadari wa vita waheshimiwa sana na wake zao warembo waliopambwa vito wote walikuwa wameketi katika utaratibu.

⁵⁰ Na kama ilivyokuwa wakati huo, kulikuwako, loo, kitu kama uyoga uliokuwako, hilo jengo limekalia nguzo zilizochomoza, kitu kama usanifu mamboleo wa majengo, usa- . . . usanifu. Na Wafilisti hawa wote walikusanyika pale juu, nao walikuwa wamejiweka kule kwa ajili ya tukio hili kuu. Nao walikuwa kwenye tamasha hii kuu, huku macho yote yamelengwa katikati ya uwanja huu. Hapana shaka walisimama, wapate m—mtazamo mzuri kwenye tukio hili lililokuwa karibu tu kuanza.

⁵¹ Na sasa tunapoketi hapa alasiri ya leo, hebu tuone kama tunaweza, kwa mawazo ya nia zetu, tujiweke mahali hapo, ili tutazame tukio hili. Tunaona nini?

⁵² Huyu hapa anakuja, akielekea katikati ya uwanja, maskini mvulana mdogo, ameushika mkono wa kipofu, anaenda akijikwaa, akiyumbayumba. Walikuwa wamemaliza maonyesho mengi ya tumbili, na—na vitimbi vidogo, na kadhalika; bali sasa umewadia wakati wa tukio muhimu, kitu kile walichokuwa wamekingojea kwa muda mrefu sana, tukio muhimu la siku. Matangulizi yalikuwa yameisha, kumbi zilizorudisha mwangwi alasiri nzima kwa tamasha za ulevi. Kwa kuwa, walikuwa wakisherehekea ushindi wa Dagoni, samaki-mungu wao, dhidi ya sanduku na ahadi ya Yehova.

⁵³ Ni tamasha la fedheha jinsi gani, tunapoweza kuwazia kitu kama hicho kikitendeka; cha mungu-samaki wa taifa la kikafiri, likisheherekea ushindi dhidi ya watumishi wa Yehova, yote kwa sababu ya mtu kushindwa kutekeleza mambo aliyochaguliwa kufanya. Na hapa walikuwapo makafiri wanawake walevi,

wakifanya ghasia, wamepambwa vito, wamepaka rangi nyuso zao, sherehe za Hollywood mamboleo, wakimleta mtumishi wa Bwana Mungu, amefungwa pingu, kwa ajili ya tukio muhimu la alasiri hiyo.

⁵⁴ Yule kijana hapana shaka alimkokota pale, akijikwaa, huku likija umbo hili kubwa mno la mwili wa kibinadamu, uliong'olewa macho yote mawili, nywele zikining'inia chini mgongoni mwake, amefungwa na kukazwa, apate kuliburudisha kundi hilo la walevi wgomvi wasioamini. Hapana shaka aliyumbayumba hadi kwenye nguzo walimokuwa wanaenda kufanya dhihaka kuanza.

⁵⁵ Ninapowazia hilo, ninaliwazia kanisa lililochaguliwa na Mungu, kumfanyia Mungu jambo fulani. Nalo likamwachilia adui kuyapofusha macho yake kutoka kwenye Neno la Mungu aliye hai na Amri za Mungu, na jukumu lililochaguliwa na Mungu kutekeleza; likaishia tu kuwa tamasha katika mahali pa kujificha pa wanawake walevi, waliopodoa nyuso, wakavikwa vito, huku wamevaa kaptura, wamekata nywele zao, pamoja na wanaume wa kilimwengu. Kanisa linalopaswa kuwa likiangaza katika mamlaka na nguvu za Bwana! Ni fedheha jinsi gani!

⁵⁶ Jinsi hapana shaka ilikuwa ni aibu kwa Samsoni! Pamoja na mwili wake wote ulioandaliwa, uliokuwa unaweza hata na zaidi, na alikuwa amethibitisha Mungu alitumia nguvu Zake kupitia mwili wake. Na kila msuli aliowahi kuwa nao, ungali ulikuwa mwilini mwake, ila baraka za Bwana zilikuwa zimemwacha.

⁵⁷ Huenda tukawa na mwili wetu wote. Huenda tukawa na kaida zetu za kidhehebu. Huenda tukaandika majina yetu kwenye makaratasi na kwenye madaftari. Lakini sijui, leo hii, kama kanisa la Kipentekoste halisimami karibu mahali pale pale, huku macho yake yameng'olewa kutoka kwa Neno la Mungu, na kwa kusudi alilolifia Yesu, kusudi sote pamoja tuweze kushiriki kwenye Neno na mambo ya Mungu.

⁵⁸ Aibu, aliipata, katikati ya wakati alioishi. Ninapomwona Samsoni amesimama pale, ni mfano, mfano wa taifa lililoanguka, lililopotoka kimaadili, na kanisa lililoanguka kimaadili, lililopotoka. Maana, yeye aliwakilisha Israeli kama taifa, na nguvu za Mungu pia, ambazo mahali pake ni kanisani. Hakika ilikuwa ni tamasha ya kusikitisha, tunapomwona amesimama pale. Hata hivyo, kuletwa kwake huko nje, na huyu kijana akimwongoza, huku hana macho.

⁵⁹ Kama adui anaweza tu kuyapofusha macho yako usije ukaliona jambo halisi la Mungu, utatembea moja kwa moja juu yake na usilijue. Haidhuru Mungu anafanya nini, na kulithibitisha kwa Maandiko Yake, na kulihakikisha kwa nguvu Zake; kama macho yako hayajafunguliwa kuyaona mambo ya Mungu, utatembea moja kwa moja juu yake kipofu uwezavyo kuwa.

⁶⁰ Basi yule pale amesimama. Kwa hiyo hapana shaka ulikuwa ni wakati wa kushtusha sana, wakati askari hawa walevi pamoja na wanawake, wakiwa na bilauri zao za kokteli mkononi mwao. Ninaweza kuzisikia zikirudisha mwangwi ukumbini, “Ati huyu ndiye Samsoni, yule shujaa wa Mungu, shujaa wa vita, yule askari mashuhuri,” amesimama katika hali hiyo. Ningewazia, kupitia kwa hao askari wakati wakisimama huku wamewakumbatia wapenzi wao wa Hollywood mamboleo, na zali zao nzuri za vito zikiliza njuga, wafuasi wa kanisa hili kubwa la Dagoni. Nawazia wengine wao wangepoteza kukumbuka, kwamba kwa jina la Samsoni, jina lake lenyewe liliwatetemesha. Jina lake lenyewe lilisababisha—lilisababisha woga juu yao, kwa kuwa alikuwa amepakwa mafuta na Mungu. Wengi wao walikumbuka hilo.

⁶¹ Wengi wao hao askari wakisimama pale, wangepoteza kukumbuka wakimwona amesimama na mfupa wa taya la nyumbu mkononi mwake, Wafilisti elfu moja waliokufa wamelala pale. Ingetendekaje? Wakati mfupa wa taya la nyumbu ulipotwaga moja ya hizo kofia za chuma, yenye upana wa inchi moja na nusu hasa, ya shaba tupu; mbona, ukiitwaga kofia hiyo ya chuma kwa mfupa wa taya la nyumbu, taya hilo la nyumbu lingeruka litawanyike maelfu ya vipande. Lakini Samsoni, huku nguvu za Mungu zikiwa juu yake, aliwaangusha Wafilisti elfu moja, akizivunja ngao zao na kuziweka kwenye... miguu yake. Ningewazia wengi wa hao askari waliokuwa wametoroka wakati huo, walisimama pale nyuma na kukumbuka. “Ati yule ni Samsoni?”

⁶² Walikumbuka wakiuona ule mfupa wa taya la nyumbu mkononi mwake, na kusema, “Ni nani mwingine anayetaka kuonja huu kidogo?” Alikuwa ni mtu ambaye aliweza kuzungumza. Alikuwa ni mtu aliyepakwa mafuta na Mungu. Mungu aliahidi kumbariki. Alikuwa katika nguvu za Yehova.

⁶³ Loo, hapana shaka wapo wengi hapa wanaoweza kukumbuka huko nyuma wakati kanisa liliposimama katika nguvu za aina hiyo, lakini sasa lote limevunjika. Kila namna ya madhehebu, moja likipigana na lingine. Mikutano ya maombi ya kale ya usiku kucha haisikiki tena. Mikutano ya mitaani imetoweka kabisa. Imepitwa na wakati. Hata hivyo, tuna muundo wetu, tunao mwili, lakini Mungu wa miujiza yuko wapi? Kusema kweli, wengi wanamkana Huyu, hata wanakana uponyaji wa Kiungu, wengi.

⁶⁴ Papa hapa katika mkoa huu, nilikuwa na m—mtu wa kanisa, mwenye kanisa kubwa, kasema. Nilitaka kuchukua viti fulani, niviweke hapa Hot Springs, kwenye Armory nilipokuwa hapa, mimi na Ndugu Moore. Na mtu Mpentekoste kasema, “Nisingeruhusu hata...” Asingeniruhusu kuvichukua viti hivyo. Akasema, “Nisingemruhusu mtu yeyote kuketi kwenye viti vyangu, aliyeamini katika uponyaji wa Kiungu.”

Hiyo si hapa tu; ni kila mahali. Kuna shida gani? Upendeleo, kwa sababu ya udhamini na madhehebu mengine, wakisahau ya kwamba sisi ni watu wa Mungu kwa Kuzaliwa. Samsoni alikuwa amesahau hilo, pia. Ningekumbuka . . .

⁶⁵ Nadhani, wakati alipokuwa amesimama pale, kulikuwako na baadhi yao waliokumbuka usiku ule huko Gaza, jinsi ambavyo mtu huyo angeyanyanyua malango ya Gaza, ayaweke juu ya mabega yake, walipojaribu kumzingira ndani.

⁶⁶ Huwezi kuufungia ndani kwa uzio upako wa Mungu. Hakuna dhehebu linaloweza kuushikilia. Mungu huwaokoa wale ambao amewaita. “Wote alionipa Baba watakuja.”

⁶⁷ Vema, walidhani walikuwa wamemzingira ndani. Ndipo akayanyanyua malango hayo na kuyaweka mabegani mwake, akaondoka akitembea, akapanda juu ya kilima akaketi chini. Malango makubwa ya shaba ambayo yangekuwa na uzito wa tani kadhaa, na ma—maskini mtu mdogo akayang’oa kutoka kwenye miamba, akayakunja na kuyalaza begani mwake, kisha akapanda juu ya kilima pamoja nayo; wakati chochote kilichomzuia Mungu.

⁶⁸ Wengi wao katika ghasia hizo za ulevi wangeweza kukumbuka hayo juu ya Samsoni. Lakini kulikuwa na shida gani leo, hakufanya hivyo? Hapo alisimama Samsoni, bali Roho wa Mungu hakumjilia tena. Hakutiwa upako. Alikuwa amevuliwa nguvu hizi, na mwanamke aliyemshawishi akaziacha Amri za Bwana.

⁶⁹ Sijui, leo hii, kama hicho si kitu kama makanisa yetu. Mnaona? *Mwanamke*, katika Biblia, anawakilisha “kanisa.” Nami nashangaa kama hatujasikiliza ushawishi wa madhehebu mengine, tukajaribu kuwaelimisha wahudumu wetu katika Sha—Shahada ya Sanaa, kusudi kusanyiko letu liweze kusema, “Mchungaji wetu ana B.A., D.D., ama L.D.” Sijui kama hatujapotoka kwenye hamaki kuu ya ghafla, kujaribu kujenga kanisa ambalo ni bora kidogo kuliko la Kimethodisti ama la Kipresbiteri? Tungekuwa afadhali katika misheni fulani, huku Roho wa Mungu akiwa juu yetu, kuliko vile tungekuwa katika hali hii. Sijui kama hatujawinda waongofu na kuvutiana sisi kwa sisi, kujaribu kuyapanua madhehebu yetu? Na tuna, tuna mijengo mikubwa, lakini Roho wa Bwana yuko wapi?

⁷⁰ Hapo alisimama, amevuliwa na mwanamke. Ni kitu gani hapana shaka kilipitia niani mwa mtu huyo wakati aliposimama pale? Alikuwa na wakati wa kuyatafakari.

⁷¹ Natumaini kanisa litapata muda mwingi kama huo. Ni kitu gani kilicho cha zaidi kwako, milioni moja zaidi ama kilindi kikubwa zaidi cha baraka za Mungu nafsi mwako? Tumetafuta . . .

⁷² Na tungeweza kuwa na mambo mengi zaidi ambayo nimeandika hapa, juu ya hao majemadari na kile Samsoni alichofanya, yale waliyokuwa wakiwazia.

⁷³ Sasa hebu tushuke twende kwa Samsoni. Basi unafikiri ni kitu gani kilichokuwa kinapitia niani mwake, juu ya ushindi mwingi aliokuwa amepata, mambo mengi makubwa aliyokuwa amefanya wakati Roho wa Bwana alipokuwa juu yake? Lakini alijua ya kwamba alikuwa na kila msuli, bali Roho wa Bwana hakuwako.

⁷⁴ Hebu niwaambieni jambo fulani, enyi kanisa. Usijaribu kujiunga na kanisa lenye madoido kuliko yote, kundi lenye ufasaha mwingi kuliko yote. Wewe dumu na Kristo, alipo Roho wa Bwana.

⁷⁵ Ndipo hapana budi aliwaza juu ya ule ushindi mkuu aliokuwa amepewa na Mungu, na wa nyakati ambapo macho yake yalikuwa yamefunguliwa, hata angeweza kuona ahadi za Mungu. Lakini sasa, kwa kuwa amenaswa katika kitu hiki, macho yake yameng'olewa.

⁷⁶ Watu wengi sana, leo hii, hushikwa katika ndoto za kiakili, kamwe hawawazii kuyachunguza Maandiko, waone kama ni kweli au si kweli. Wengine hujaribu kusema, "Haileti tofauti yoyote."

⁷⁷ Paulo, katika Matendo 19, alifikiri ilileta tofauti. Naye akasema, "Kama Malaika kutoka Mbinguni alihubiri jambo lingine lolote, Huyo na alaaniwe." Mnaona? Mnaona? Kweli inaleta tofauti.

⁷⁸ Sasa tunamwona Samsoni amesimama pale, jinsi anavyowazia juu ya mambo aliyofanya wakati mmoja na Ufalme wa Mungu. Na jinsi ambavyo Mungu. . . Yeye alikuwa amempungukia Mungu, na alikuwa amewaaibisha watu wa Mungu. Naam, bwana. Sasa yeye ni mfungwa wa taifa lile lile ambalo Mungu alimwinua apate kuliangamiza.

⁷⁹ Ninataka kutulia hapa kwa dakika moja. Pentekoste, mnajua ninawapenda. Nilipowajia, Jack Moore, Richard T. Reed, Ndugu G. H. Brown, Ndugu Ben Pemberton, na watu wengine mashuhuri, kutaka kujua mambo mliyokuwa nayo, ilionekana tulikuwa na mengi sana shirika mpaka tulikuwa kama glavu inayoenea mkononi; nilitoshea na nyinyi kabisa. Kwa ajili ya Ujumbe, bila kujua kulikuwako na kanisa kama hilo, nililoliamini, hili hapa lilikuwa ni kundi la watu lililo tayari kuupokea Huo. Ningali ni Ndugu Branham. Ningali ndugu yenu, nami nawapenda.

⁸⁰ Lakini je! mnatambua, kitu kile kile ambacho Mungu aliwainua kwa ajili yake, mmejisalimisha kwake. Mungu aliwatoa kwenye hayo madhehebu, miaka kadhaa iliyopita, apate kufanya watu kutoka kwenu, nanyi mkageuka

mkakiundia dhehebu kitu kile tu Mungu alichowatoa kwake mpate kukiasi.

⁸¹ Ninamsahi mtu yeyote anionyeshe mahali popote katika hisotria, tangu kanisa lilipojiundia dhehebu kwa mara ya kwanza, ambalo lilikuwa ni kanisa Katoliki la Kirumi, huko Laodikia, ama Nikea, hasa, Rumi, wakati kanisa Katoliki lilipounganishwa na kufanywa dhehebu. Na hivi kanisa lolote tangu Martin Luther, upande huu . . .

⁸² Hapo Mungu alipompa Martin Luther ufunuo wa kuhesabiwa haki; na, mara Luther alipoondoka, walilifanyia dhehebu, nalo likaanguka. Moja kwa moja akaja Wesley, baada yake, na Asbury, na kadhalika, wakaondoka; wakaliundia dhehebu, nalo likaanguka. Moja kwa moja akaja Alexander Campbell, nalo likaanguka, kwa dhehebu. John Smith akafuata, kwa ajili ya Baptisti, nalo likaanguka. Na kila wakati ambapo mwanadamu amejaribu kufanyia jambo fulani utaratibu, wa mfumo wa kujibunia, lilianguka na kamwe halikuinuka tena. Hamna historia yoyote, mahali popote, ambapo kanisa lolote lililopata kuundiwa dhehebu, ila lililoanguka, na kila moja lililoanguka, halikuinuka tena.

⁸³ Wana wa Israeli, katika mfano, walipaswa kuifuata ile Nguzo ya Moto. Na kila usiku hawana budi kuwa tayari, sio kujiundia dhehebu na kuketi chini hapa, bali kuambatana na ule Moto.

⁸⁴ Hivyo ndivyo Mungu anavyowataka watu Wake kufanya, kuambatana na Roho, kufuatana na wakati!

⁸⁵ Mnasema, “Vema, Ndugu Branham, tumekuwa na kila namna ya mvua, na mvua za ndani na mvua za nje.” Ninyi mna akili. Sijali ni ufunuo wa aina gani, na jinsi unavyoonekana mzuri, kama haulingani na Neno la Mungu, achana nao. Hii ndiyo ramani ya kupitia nyikani, Neno la Bwana.

⁸⁶ Lakini hili hapa kanisa limesimama leo hii, kanisa la Kipentekoste, katika yapata madhehebu ishirini ama thelathini mbalimbali, kila moja likiliita lingine, *hiki, kile, na kinginecho*, “banda la mwewe,” na kadhalika. Ni fedheha jinsi gani, wakati kitu kile kile kilichomfanya Mungu kuwavuta mtoke kwenye madhehebu hayo, mligeuka na kufanya jambo lile lile walilofanya. Hivyo ndivyo Samsoni alivyofanya hasa. Mungu alimwinua Samsoni apate kuliangamiza taifa hilo. Naye Mungu aliwainua mpate kuwa watu maalum, sio dhehebu.

⁸⁷ Lakini wakati Mungu alipoanza kuwatoa Israeli kutoka ninii . . . kutoka Misri, walikuwa tu yapata safari ya siku kumi kutoka nchi ya ahadi, yapata maili arobaini. Lakini walikaa nyikani kwa muda wa miaka arobaini. Kwa nini? Neema ilikuwa imewapa mwana-kondoo kwa ajili ya dhambi zao, tohara ya ishara, Nguzo ya Moto kama ushahidi, Musa kama nabii. Neema

ilikuwa imewapa kila kitu walichohitaji, bali walitaka jambo la kufanya wao wenyewe.

⁸⁸ Hawakujua hata kidogo, wakati Miriamu alipokuwa akicheza na tari, huku wana wa Israeli wakicheza pamoja naye, naye Musa akiimba katika Roho, walikuwa tu na siku kumi wafikie nchi kamili iliyoahidiwa. Hawakujua hata kidogo, miaka arobaini, nayo mizoga yao ingeozea nyikani. Ni nini kilichoisababisha? Israeli ilifanya uamuzi wake wa kipumbavu kuliko yote iliyopata kufanya, hapo ilipokubali torati badala ya neema, hapo walipotaka kufanya maaskofu kadhaa na kitu fulani chao wenyewe, kitu kilichowabidi kufanya katika hayo. Mungu alikuwa katikati yao, akiwaongoza.

⁸⁹ Na hivyo ndivyo Pentekoste ilivyofanya hasa. Wakati Mungu alipofunua kitu fulani kipya katika Maandiko, badala yake walikiita hoja mpya ama chochote unachotaka kufanya juu yake. Lakini wakati Mungu alipofunua jambo fulani, badala ya kuikubali Kweli na kuijaribu Hiyo kwa Biblia, walijiondoa na kuunda dhehebu, wakajitenga wenyewe. Ndipo likaja *hili, lile*, na lile *lingine*, na sasa mnasimama mmeopotoshwa, kanisa la Kipentekoste, limefungwa katika pingu za kimadhehebu. Kitu ambacho Mungu aliwainua mkakiangamize, na sasa ninyi mmejiundia tu dhehebu kama walivyo. Wanaume wataua katika kila moja yao, na wanawake; hiyo ni kweli, kila moja yao.

⁹⁰ Na sisi, kila mmoja wetu, ana hatia. Nyungu haiwezi kuiita birika nyeusi. Sisi sote tuna hatia, kila mmoja wetu, nyinyi wa umoja, uwili, utatu, na—na lolote uwezalo kuwa. Ni fedheha jinsi gani! Ni shutuma jinsi gani mliloleta juu ya Yesu Kristo! Ni lawama jinsi gani kwa jina la Pentekoste! Wameleta shutuma nyingi sana hata karibu, limekuwa ni jina la aibu. Watu karibu hawataki kujihusisha na jina kama hilo. Ni kwa sababu kwamba mlifanya yale ambayo hamkupaswa kufanya. Na kuendelea na kuzifuatia amri za Bwana, linapaswa kuwa ni kundi moja kubwa la Mungu, likielekea taratibu kwenye ushindi, leo hii.

⁹¹ Alimwacha mwanamke amshawishi amtote kwenye Neno la Mungu, sasa amesimama akifanya vitimbi kwa ajili ya shetani. Hiyo ni kweli. Kweli kabisa.

⁹² Jambo lile lile linatendeka leo hii, kumwacha Yezebeli, “mama wa makahaba.” Ufunuo 17 inasema kwamba alikuwa “mama wa makahaba.” Sasa, kama yeye ni kahaba, huyo ni—huyo ni mwanamke asiye mwaminifu kwa mumewe. Anadai Kristo ni Mumewe, wala haishi kwa Amri Zake.

⁹³ Nayo makanisa hayo mengine yanafanya nini? Kahaba ni kitu gani? Ni kitu kile kile kama huyo mwingine. Ni kitu gani? Umalaya kwa Neno la Mungu. Naye alikuwa ni “mama wa makahaba.” Na kuliachilia hilo fundisho la Yezebeli, na kadhalika, kwa sababu kundi la watu wenye akili, wanaotaka kukusanyika na kujiundia kitu fulani kusudi wapate majina

makubwa wenyewe. Na hilo hapo kanisa limesimama, udugu uliogawanyika. Loo, ni, ni fedheha jinsi gani usiku wa leo!

⁹⁴ Ni jambo la kuchukiza jinsi gani, vipofu kiroho. “Loo,” unasema, “vema, mimi si kipofu kiroho.” Matendo hunena kwa sauti kuu kuliko maneno; inathibitisha kwamba wewe ni kipofu kwa jinsi unavyojikwaa kwenye vitu. Unaona?

⁹⁵ Sasa, kumbukeni, kanda hii inatengenezwa na itasambazwa kote ulimwenguni. Mnaona, na zaidi sana sizungumzi papa hapa, lakini hii inaenda kwenye yapata mataifa kumi na saba mbalimbali, huko nje misituni na kila mahali.

⁹⁶ Vipofu kiroho! Vipofu kwa kitu gani? Neno la Mungu, kweli ya Mungu. Dhehebu lako halitaruhusu. . .

⁹⁷ Wahudumu wazuri ambao hunijia, na kusema, “Ninaamini hilo kuwa ni Kweli, Ndugu Branham, bali kama nikihubiri Hilo. . .” Sasa, haya basi. “Kama niliamini Hilo, vema, hao watu wangeninii. . .”

⁹⁸ Sijali kile watu wasemacho, sijali kile dhehebu lisemacho; ni kile ambacho Mungu alisema kwamba ni Kweli. Na kama ni Kweli ya Mungu, Mungu ataiunga mkono. Mnawezaje kutarajia kuwa na imani wakati mna shauku ya kuheshimiana ninyi kwa nyinyi? Mnaona, inawaondolea imani.

⁹⁹ Ilirudi kwenye madhehebu, ile Pentekoste iliyozaliwa nje ya dhehebu. Pentekoste haikuzaliwa ndani ya dhehebu; ilizaliwa *nje* ya dhehebu. Ndipo ujanja wa Shetani ukawavuta moja kwa moja kurudi ndani yake, mahali mlipotoka, “Kama nguruwe alivyoondea kugaagaa kwake, na mbwa kwenye kugaagaa kwake.” Sasa hebu waangalieni, wameshindwa!

¹⁰⁰ Inatupasa tayari tuwe kwenye nchi ya ahadi. Yesu Kristo anapaswa kuwa maarufu sana miongoni mwetu, hata kusingekuwako na maradhi yoyote. Loo, lingekuwa ni tukufu.

¹⁰¹ Hakupaswi kuwako na wanawake waliokata nywele zao, wanaovaa nguo fupi. Na—na hakupaswi kuwako na wanaume walioa mara tatu ama nne, mashemasi kanisani mwetu. Na msiniambie hayako katika Pentekoste; hakika yapo. Lakini ni kwa sababu ya hadhi ya kijamii. Haipaswi kuwa, bali liko. Kwa nini? Kwa sababu ya mivuto ya kimadhehebu, siasa, fedha, badala ya kuambatana na Neno. Kumfukuza ndugu fulani wa thamani, na kumweka mtu fulani kwa sababu ana hadhi kuu ya kijamii mjini.

¹⁰² Ninataka mtu aliye na hadhi ya kijamii Utukufuni. Kama hajui ABC zake, inaleta tofauti gani? Je! mnajua maana ya ABC? Daima mwamini Kristo. Hiyo ni kweli. Mnajifunza hilo.

¹⁰³ Mtu fulani alinijia, si muda mrefu uliopita, na kasema, “Ndugu Branham,” ninii sana. . .mmoja wa wahudumu Wapentekoste maarufu sana nchini. Alinipeleka chumbani mwake, akasema, “Ninataka kukuombea.”

Nikasema, “Mimi si mgonjwa.”

Akasema, “Na—nakupenda.”

Nikasema, “Huo huhisiwa pande zote mbili.”

¹⁰⁴ Akasema, akaniambia, akasema, “Kwa nini usiache kuwaambia hao wanawake kuhusu nywele zao zilizokatwa na upuuzi huu wote wa namna hii, na kuhusu kanisa?” Kasema, “Hiyo si kazi yako.”

Nikasema, “Ni ya nani basi?”

¹⁰⁵ Akasema, “Itakuja kutimia kwamba hutakuwa na kitu ila lundo la nguzo kuhubiria.”

¹⁰⁶ Nikasema, “Afadhali nifanye hilo na kuihubiri ile Kweli, kuliko kupatana na ibilisi.” Unaona? Unaona?

¹⁰⁷ Akasema—kasema—kasema—kasema, “Ndugu Branham, hivi Mungu hakukuita kuwaombea wagonjwa?”

Nami nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Watu wanakuamini wewe kwamba ni nabii.”

Ndipo nikasema, “Vema, hilo—hilo, kamwe sikusema hilo.”

¹⁰⁸ Akasema, “Lakini wanakuamini namna hiyo.” Basi akasema, “Kama wewe ni nabii, kwa nini usiutumie wakati wako ukiwafundisha watu jinsi karama za kiroho, na jinsi ya kuwaponya wagonjwa, na—na jinsi ya kufanya haya, kupata karama hizi za kiroho, na kulisaidia kanisa badala ya daima kusimama, ukiwagombanisha wanawake hao, na kuwagombanisha wanaume, na mambo kama hayo?” Kasema, “Vema, kwa nini usiachane nao?” Kasema, “Kwa nini usiwafundishe kitu kikubwa zaidi ya nywele zilizokatwa na upuuzi huo, na kuachana na hilo?”

¹⁰⁹ Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawazijui ABC zao? Hiyo ni kweli. Acha wajifunze ABC zao kwanza.”

¹¹⁰ Mhudumu mmoja mzee alienda akahubiri kuhesabiwa haki kwenye uamsho fulani, usiku wa pili, usiku wa tatu, usiku wa nne, usiku wa tano. Mashemasi wakamwita nje, na kusema, “Kasisi, hivi hujui zaidi ya mahubiri juu ya kuhesabiwa haki?”

¹¹¹ “Loo, hakika. Bali acheni wote wapate kuhesabiwa haki kwanza, ndipo tutahubiri kitu kingine.” Hiyo ni kweli.

¹¹² Loo, laiti ungalirudi tu kwenye msingi! Hapo alisimama Samsoni, ameshindwa.

¹¹³ Sasa angalieni, huenda tukawa warembo zaidi, hilo huenda likawa hivyo. Lakini ni kama tu nilivyokuwa nikiteremka barabarani hivi majuzi, niliona ubao mkubwa wa matangazo, uliosema, “Mahindi chotara, ya Funk,” jinsi yalivyokuwa ni makubwa sana. Bali si mazuri. Ni mabaya tu yawezavyo kuwa, na yanaliangamiza taifa. Mlisoma habari zake, Reader's Digest,

“Kama wanawake wataendelea kula nyama chotara na mahindi, na kadhalika, hawawezi kupata mtoto katika muda wa miaka ishirini kuanzia sasa.” Hamna uzuri ndani yake.

¹¹⁴ Chotara ni nini, mmea wa tuta? Kama si mmea asili, huna budi kuendelea kuunyunyizia wakati wote, ili kuukinga na vijidudu. Vijidudu vitaula. Lakini kama ni mmea wa asili, haikubidi kuunyunyizia. Mmea mzuri wenye afya, kijidudu hakitatambaa juu yake.

¹¹⁵ Hiyo ndiyo shida, inakubidi kuendelea kuwabembebeza watu kanisani, “Utukufu kwa Mungu, dada,” unaona. Wewe ni chotara, umeingizwa kwa njia nyingine.

¹¹⁶ Ukichukua mahindi hayo chotara ukayapande tena, basi utapata nini? Hakuna kitu. Hata hayatafanya chochote.

¹¹⁷ Kanisa ni malidadi leo hii, hiyo ni kweli, mijengo mikubwa kuliko mliyowahi kuwa nayo, makusanyiko makubwa kuliko yote mliyowahi kuhubiria, wahudumu wenye akili zaidi kuliko mliyowahi kuwa nao. Mlizoea kumchukua mtu kutoka kwenye mashamba ya mahindi mahali fulani, ambaye Mungu alimwita huko nje kwenye maeneo ya vichakani. Bali sasa mmewatuma watoto wenu shuleni, na kufanya wajukuu kutokana nao, kisha wakarudi na ma-Ph.D yote, na LL.D. Na hata moja la makanisa makubwa ya Kipentekoste leo hii, kabla hawajamtuma mtu kwenye huduma ya kimishenari, hana budi kusimama mbele ya mtaalamu wa akili waone kama ana bongo lenye akili kutosha. Wazia hilo!

¹¹⁸ Katika Pentekoste, masharti hayakuwa ni majaribio ya akili, yalikuwa ni majaribio ya Roho Mtakatifu aliyeshuka chini kwenye Siku ya Pentekoste. Hilo haliwaziwi na watu leo hii.

¹¹⁹ Hivi mlijua kanisa Katoliki la Kirumi kwanza lilikuwa ndilo kanisa la Kipentekoste la asili? Ililichukua miaka elfu mbili kufikia hali liliyofikia leo hii. Kama dhehebu hili la Kipentekoste likiendelea miaka mingine hamsini, litakuwa baya kuliko kanisa Katoliki. Hiyo ni kweli. Dhambi inalundikana kila upande! Sasa huenda msifikiri ya kwamba mimi. . . Huenda mkafikiri mimi nina kichaa, bali ninajua nilipo. Mnaona? Na ni kweli. Hebu ngojeni tu na mtaona. Naam.

¹²⁰ Chotara, mahindi chotara, yakiwafanya wanawake wembamba viunoni na wapana mabegani, na kadhalika.

¹²¹ Mageuzi ya kuendelea yalikuwa yakitwambia kwamba, katika mageuzi, ya kwamba wanyama fulani waliungana wakazaa kitu tofauti, na kitu tofauti, hata ikamfikia mwanadamu. Waliendelea kufanya utafiti kote hata wakaikataa nadharia yao wenyewe.

¹²² Hebu niwaambieni jambo fulani, ninyi wakulima hapa. Ni kitu gani kinachomfanyiza nyumbu? Yeye ndiye mnyama wa kuchukiza kuliko wote ulimwenguni. Yeye ni chotara. Hana

akili kabisa, kwa kuanzia. Huwezi kumfundisha chochote. Atangojea maisha yake yote, apate kukupiga teke kabla hajafa. Huwezi kumwambia chochote. Ni kitu gani? Kwa sababu yeye ni chotara.

¹²³ Inanikumbusha tu juu ya Wakristo wengine machotara, wanavyojiita. Unaweza kujaribu kumwambia maskini nyumbu kitu fulani, yeye atasimama ameyainua masikio yake, alie, “Hoo! Hoo! Hoo!” Mnaona? Yote ajuayo ni kulia na kupiga makelele. Huwezi kumwambia ukweli na kumfundisha chochote. Hivyo ndivyo walivyo watu hawa. Ukiwaambia juu ya Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, “Hoo! Hoo! Siku za miujiza zimepita,” mlio wa seminari fulani tuliojifunza. Ni chotara.

¹²⁴ Roho Mtakatifu ataitikia kila amri ya Mungu kwa “amina.” Hiyo ni roho fulani ya seminari ikipumua kutoka kwake. Sio kupiga makelele dhidi ya Neno la Mungu, kama ni Roho Mtakatifu. Ataliitikia “amina.” Mnaona?

¹²⁵ Mwajua, nafikiri nyumbu ni ujinga. Lakini mnajua nini? Yeye hawezi kusema baba yake alikuwa ni nani au aliyekuwa mama yake. Mnaona, baba yake alikuwa maskini punda dume, mama yake alikuwa farasi jike, bali hawezi kuzaa tena. Amekwisha.

¹²⁶ Mmea hauwezi kujizaa tena. Hebu chukua waridi jeupe na waridi la samawati, utaleta waridi lako la urujuani; upande mara mbili au tatu, litatokea jeupe ama la urujuani, unaona.

¹²⁷ Hiyo inathibitisha, unaona, kamwe hayatokei namna hiyo. Mungu alisema, “Na kila kitu kizae kwa jinsi ya mbegu yake,” na hivyo ndivyo inavyobakia. Mtu alifanywa katika sura ya Mungu, sio tumbili. Mnaona? Jambo hilo la kiwazimu!

Angalieni, mwajua, ujinga wa nyumbu. Lakini mnajua nini? Huwezi kumwambia chochote. Yeye ni kichwa ngumu.

¹²⁸ Lakini nafikiri farasi ukoo safi halisi, loo, jamani, yeye anajua mama yake alikuwa ni nani, baba yake alikuwa ni nani. Yeye ni asili safi. Anajua babu zake wote na kila kitu, kwa kuwa ana ukoo safi.

¹²⁹ Hivyo ndivyo ilivyo kwa hawa machotara, wanaojiita Wakristo. “Siku za miujiza zimepita. Vema, sisi Wapresbiteri, sisi Wamethodisti, sisi *fulani wa-fulani*, hatuamini *Hili*. Sisi Wa utatu, sisi *nanii-wa-nanii*, hatuamini. Hatufanyi *hili*.” Mnaona, hujui mahali unaposimama.

¹³⁰ Lakini Mkristo ukoo safi aliyezaliwa mara ya pili kutoka kwenye Kitabu cha Matendo, anajua hasa mahali anaposimama. Yeye amezaliwa kwa Roho, na hii *hapa* nasaba yake. Anatoka kwenye tawi la Mungu. Litazaa kitu kile kile kila wakati.

¹³¹ Si ajabu, kanisa lina sura nzuri zaidi. Lakini kuna nini? Limepungukiwa na Roho. Limezaa likamaliza, kwa ulimwengu. Linawaacha wanawake wavae kaptura. Wacheze kinanda,

linawaachilia wajipodoe. Linawaacha wanaume waoe mara nne ama tano, na kushikilia mahali pao, wadhifa. Mambo haya yote ya namna hiyo wanayopitia, vile hasa Maandiko yalivyosema. Limeshindwa tu kama Samsoni alivyoshindwa. Vivyo hivyo hasa. Naam, bwana.

¹³² Loo, kama Samsoni alivyowazia! Huenda mimi... Sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi; nitayaruka baadhi ya mafungu haya hapa. Kama vile Samsoni hapana budi alisimama pale na kutafakari juu ya kosa lake, na mahali angalikuwa!

¹³³ Kumbuka Israeli. Naweza, mtaniwia radhi kidogo, kurudi kwa Israeli? Mnajua nini, walifanya nini miaka hiyo arobaini wakati walipojiundia dhehebu lao kule nje? Badala ya kwenda moja kwa moja, wakiongozwa na ile Nguzo ya Moto, Malaika wa Bwana, ambaye alikuwa ni Kristo, badala ya kwenda moja kwa moja na kumfuata Yeye. Katika yapata siku kumi, wangukuwa kwenye ahadi kamili. Bali mnajua nini, "Walitangatanga nyikani," Biblia ilisema.

¹³⁴ Wakafikia Kadeshi-barnea, ambayo ilikuwa ni kiti cha hukumu, na hapo wakati wale wapelelezi waliporudi na kuzungumza juu ya nchi hiyo. Wao walisema, "Hatuwezi kufanya hivyo."

¹³⁵ Kalebu na Yoshua wakasema, "Tunaweza hata na zaidi kufanya hivyo," kwa kuwa walikuwa wakiitazama ahadi ya Mungu, si vile hali za mambo zilikuwa.

¹³⁶ "Hatuwezi kuwa na kanisa pasipo kuwa na dhehebu." Vema, hamwoni yale Mungu alisema. Hiyo ni kweli.

¹³⁷ Walifanya nini? Mungu aliwabariki? Hakika, hakika. Walitangatanga. Walioa wake. Walipanda mashamba ya mizabibu. Na wakazaa watoto, na wakaongezeka. Nao walifanikiwa nyikani. Hiyo ni kweli. Lakini bado hawakuwa wameingia kwenye baraka kamili.

¹³⁸ Kwa hiyo wakati hawa wote waliofanya kundi hili kubwa mno la madhehebu, "wapiganaji wa kale" ndivyo liliitwa, vema, Mungu aliwaacha wakae kule mpaka kila mmoja wao akafa. Ndipo Yeye akaanza na kizazi kipya, chini ya uongozi wa Yoshua, ambaye aliliamini Neno, amina, naye akawapeleka kwenye nchi ya ahadi.

¹³⁹ Ee Mungu, jalia kizazi hiki kichanga cha Wapentekoste ki—kipate ono. Mnaona, walienda moja kwa moja kwenye nchi ya ahadi. Tunapaswa kuwa mahali ambapo tuna kila namna ya karama za Mungu.

¹⁴⁰ Kweli tulinena kwa lugha. Hiyo ni kweli. Hiyo ni sawa. Sina chochote dhidi ya hilo. Musa alivuka Bahari ya Shamu; adui akauawa nyuma yake. Tu—tu—tunathamini hilo. Lakini hilo bado si lote la hayo.

¹⁴¹ Baba na mama zenu hawakuwazia kabisa walipokuwa wamesimama huko nje na kuwalenga kwa bastola kupitia madirishani, nao huku wanacheza katika Roho, kwamba watoto wao kamwe wangefikia jambo hili? Lakini walilifikia.

¹⁴² Bali kuna kizazi kipya kinachojitokeza sasa. Nywele za Samsoni zimekua. Mnaona?

¹⁴³ Angalieni! Kamwe msimwache Delila awasokote awarudishe katika kitu kama hicho. A-ha. Kaa mbali nacho. Hicho ndicho kitu kilichowalaani ninyi. Mliinuliwa mpate kukihukumu. Nami nimejaribu niwezavyo kukihukumu, ingawa nimesimama peke yangu. Lakini nimejaribu niwezavyo kusimama kwenye Amri za Mungu. Ninaliona kanisa limesimama pale, limevuliwa nguvu za Mungu, limevuliwa baraka, likavuliwa karama.

¹⁴⁴ Naye Mungu ataishusha karama Yake chini. Wanasema wanasema, “Huko ni kusoma mawazo, telepathia ya kiakili,” wakati wanapaswa kuwa wakiikumbatia Hiyo. Mnaona? “Vema, yeye yuko kwenye wa Umoja sasa. La, hiyo ni, huenda hiyo ikawa, kwa kuwa, loo, walikuwa *hivi, vile*, ama *vinginevyo*.” Mnaona? Loo, laiti mngalijua tu siku yenu! Msiiache Hiyo iwapite. Hii ndiyo saa, kuunganika ndani ya Kristo. Angalieni.

¹⁴⁵ Samsoni akisimama pale, akiwazia juu ya kosa lake, mambo aliyokuwa ameyafanya. Sasa mnatambua ni kitu gani kilichomfanya kuwa hivyo? Adui aliyang’oa macho yake.

¹⁴⁶ Na hilo ndilo jambo la kwanza dhehebu litafanya, litayapofusha macho yako usione ushirika wowote mwingine ila walio wenu wenyewe. Amina. Ningeweza kusema mambo mengi sana papo hapo, bali si—sitayasema. Lakini nyinyi, kama ninyi mna nia za kiroho, mnajua ninalozungumzia. Litayapofusha macho yako! Wewe tu na kundi lako; kama wewe ni Mmethodisti, wewe ni Mmethodisti tu; kama wewe ni Mbaptisti, wewe ni Mbaptisti tu. Kama wewe ni Mpresbiteri, wewe ni... Kama wewe ni wa Umoja, kama wewe ni wa Uwili, kama wewe ni wa Utatu, ama ni mangapi zaidi waliyo nayo, unaona, wewe ni huyo tu. “Hayo mengine hayafai kitu.”

¹⁴⁷ Baptisti ilikuwa na msembo katika siku za mwanzoni za Billy Graham, arobaini-... “Katika ’44, milioni moja zaidi.” Mlipata nini? Kundi la wanafiki wavuta sigara, wanaojiunga na kanisa.

¹⁴⁸ Wakati Billy, mwenyewe, nilipokuwa kwenye kiamshakinywa chake, yeye alisema, “Mnajua shida yake ni nini?” Kasema, “Huu hapa mfano.” Akasema, “Nitaingia...” Kasema, “Mtakatifu Paulo alingia mjini, akampata mwongofu mmoja. Kisha akarudi, mwaka mmoja tangu hapo,” ndipo kasema, “mwongofu huyo mmoja alileta wengine thelathini.” Akasema, “Nitaingia mjini kwa majuma sita, na kupata maamuzi elfu thelathini, kisha naweza kurudi katika miezi

sita wala siwezi kupata thelathini.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁹ Vema, sasa, nilivutiwa na mtu huyo kwa ujasiri wake, bali ningetaka kumwuliza swali moja. “Ni nani aliyewachukua waongofu wa Paulo? Alikuwa na mchungaji gani mzembe karibu naye?” Ilikuwa ni nini? Paulo alikaa naye mpaka akawa mtoto wa Mungu kwelikweli, aliyezaliwa kwa Roho. Yeye alimwingiza kwenye kilindi cha Kristo sana hata asingeweza kuangalia nyuma.

¹⁵⁰ Hao huenda tu pale juu na labda wanajiunga na kanisa, ama hata kunena kwa lugha. Ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini Roho Mtakatifu hunena kwa lugha. Lakini ninajua ya kwamba wote wasemao kwa lugha hawana Roho Mtakatifu. Mnaona? Nimewaona wachawi wakinena kwa lugha, na kunywa damu kwa fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita ibilisi, wananena kwa lugha na kuitafsiri. Hilo si lisiloweza kukanushika. La, la. Uzima wa Kristo ndani yako, tunda likijishuhudia lenyewe, hilo ndilo. Lakini tunaridhika na hilo, “Kama mtu alinena kwa lugha, ni hivyo tu, acheni aingie.” Angalieni kile mlicheo nacho leo hii. Mnaona? Hiyo ni kweli, kunena kwa lugha, bali si Kweli yote.

¹⁵¹ Kama yule mtu mweusi aliyekuwa akila kipande cha tikitimaji. Alisema, “Uliionaje, Mose?” Akasema, “Hiyo ilikuwa nzuri, bosi, lakini hakika kuna nyingi zaidi ya hiyo.”

¹⁵² Kama ninaweza kunena kwa lugha, hakika kuna mengi zaidi ya Hiyo. Mnaona? Lakini tunafanya nini? Ni kama tu Israeli, waliridhika na jambo hilo moja, nao wakatangatanga nyikani sasa kwa muda wa miaka arobaini, wangali hawana mengine ya Hiyo huko katika nchi ya ahadi. Hivyo ndivyo tumefanya hasa.

¹⁵³ Samsoni akisimama pale, (sina budi kuharakisha), hapana budi aliangalia nyuma, akayatafakari mambo hayo yote. Naye huyu hapa, sababu hasa ya yeye kuinuliwa, alipofushwa. Na pale umbo lake kubwa, utaratibu wake mkubwa wa mwili wa kibinadamu, mlima wa mwili umesimama pale, misuli yake mikubwa mno, bali haina nguvu.

¹⁵⁴ Sisi hapa tumesimama leo hii. Huko nyuma wakati Wapentekoste walipokuwa wakihesabiwa kuwa wachache sana, labda watu mia nne ama tano katika taifa zima, leo hii ndilo kanisa linalopanuka upesi kuliko yote ulimwenguni. Tunaingia katika kitu gani? Kundi la wafuasi. Tukiwa na umbo letu kubwa, tunapaswa kuwa wanene zaidi mara elfu kumi kuliko tulivyokuwa tulipoanza. Nasi ni dhaifu mara elfu kumi kuliko tulivyokuwa tulipoanza, kwa kuwa tunalijenga juu ya msingi usio na mwi—mwisho, juu ya dhehebu, kitu ambacho Mungu amelaani. Basi tunaweza kujenga ka—kanisa juu ya vifusi vya Sodoma na Gomora?

155 Natumaini hamtanichukia, bali mketi tu kimya kwa dakika moja na msikilize. Mnaona?

156 Hawezi kufanya hivyo. Kile ambacho Mungu amelaani, Yeye amelaani. Basi, niweke mbali na chochote ambacho Mungu amelaani. Ninataka kile ambacho Yeye anabariki. Hiyo ni kweli.

157 Angalieni wakati aliposimama pale, akitafakari. Majemadari, waliolewa nusu, wamesimama pale, “Ninakumbuka yule mtu mashuhuri. Ninakumbuka wakati aliposimama na ule mfupa wa taya la—la nyumbu, mkononi mwake. Ninakumbuka wakati alipoyakunja yale malango ya Gaza na kukwea juu ya kilima. Nayakumbuka mambo haya yote. Wakati yule simba alipomngurumia, maskini jamaa huyo mdogo, na Roho akaja juu yake, naye akamrarua tu huyo simba vipande viwili, kwa mkono wake. Naye huyu hapa amesimama, amefungwa, na mtoto mdogo anayemwongoza kote. Naye mungu wetu, mungu-samaki Dagoni, amepata ushindi dhidi yake.”

158 Haya basi. Ulimwengu umenyemelea ukaingia ndani ya kanisa, ukapata ushindi. Umewavua nguo wanawake wetu. Umeweka shauku katika mioyo ya watu kukaa nyumbani na kuangalia televisheni badala ya kwenda kanisani na mkutano wa maombi. Kuupenda ulimwengu kumenyemelea ndani na kulichukua kanisa letu la Kipentekoste kuliendesha kuelekea kuzimuni.

159 Shauku na imani? Kumpitisha mtu upesi kwenye mstari wa maombi na kumfanya aone yale yanayotukia; kesho yake usiku, hao hapo wamerudi moja kwa moja tena. Ati Uzao wa Ibrahimu? Imani haimo. Inapaswa kuwamo, bali haimo. Wakati wewe. . .

160 Mungu alimwambia Ibrahimu mara moja, na miaka ishirini na mitano akalitazamia. Haidhuru ilichelewa jinsi gani, ninaweza kumsikia akimwambia Sara, “Nenda huko nje, una umri wa miaka sitini na mitano. Nenda kanunue jichondege kidogo, na ununue pini chache na utengeneze vijibuti. Tutampata mtoto huyo mchanga.”

“Unajuaje utampata?”

“Mungu alisema hivyo.” Na hilo lilitosha.

161 Kwanza, unaona, alikuwa amekata hedhi karibu miaka ishirini. Alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa na umri wa yapata miaka kumi na sita, kama kijana mwanamume. Haikuleta tofauti yoyote; hakuangalia hilo; hakuzingatia hilo. Alizingatia yale Mungu aliyosema. Akajitenga na kutokuamini kwote, akaenda huko nje nyikani.

162 Hiyo ndiyo shida leo hii. Unataka kujifanya pamoja na dhehebu la kutokuamini, badala ya kujitenga na mambo ya ulimwengu; unataka kuona jinsi unavyoweza kuendesha kwa karibu ukafikia mwisho wa dhambi. Angalia ni umbali gani unaoweza kukaa mbali nayo.

163 Lakini walikuwa hawa hapa. Siku za kwanza thelathini ama ishirini na nane zikapita. Kusanyiko lililochanganyikana sasa, nanyi watu wazima mnajua ninachozungumzia. “Sara, mpenzi, unajisikiaje?”

“Hamna tofauti hata kidogo, Ibrahimu.”

“Utukufu kwa Mungu, tutampata, haidhuru.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.”

164 Miaka kumi ikapita. “Ziweke hizo pini hapo, na jichondege zote.”

165 Baadhi ya rafiki zake wakapitia hapo, “Ibrahimu, baba wa mataifa, una watoto wangapi?”

166 “Utukufu kwa Mungu! Kwa wakati huu, hamna, bali nitawapata.”

“Vipi, ati wewe? Mbona, una umri wa miaka tisini.”

167 “Haileti tofauti hata kidogo. Itakuwa ni mwujiza mkubwa zaidi sasa kuliko ilivyokuwa kama ingalitimizwa huko nyuma miaka ishirini iliyopita.”

168 Lakini, leo hii, “Niliombewa jana usiku. Sijisikii vizuri zaidi leo.” Ati Uzao wa Ibrahimu?

169 Kuna shida gani? Umevuliwa. Misuli yako ya kanisa ingali pale; dhehebu lako ni mashuhuri kama la Kimethodisti ama la Kibaptisti. Unajengea msuli huu wakati wote, bali iko wapi ile imani halisi? Loo, mnapiga makofi yenu, mnapiga makelele na kuimba nyimbo, na kucheza. Jamani, nimeona hilo likitukia kwa madaktari wengi, mikutano ya wachawi, nikawaona wakipiga makofi, na kunena kwa lugha, kufasiri, na kuruka-ruka. Baba wa Kiungu ana jambo lile lile. Hilo silo jambo ninalozungumzia.

170 Ninazungumza juu ya imani halisi inayoweza kuifungua ahadi ya Mungu, na kusimama pale na kuifanya hai, jambo la Kimaandiko.

171 Waislamu, nimewaona wakianguka mitaani na kupiga makelele, “Allah, Allah, Allah,” mpaka wanapagawa sana. Na mimi pamoja na Billy Paul tulisimama pale na kumwona mtu akiutwaa upanga na kuingiza chini ya moyo wake, ndipo daktari akamwagilia maji upande *huu* yakatokea upande huo mwingine. Tukamwona akichukua ki—kipande, kama mkuki, na kukiingiza mdomoni mwake kikapitia puani mwake, na hatatokwa na hata tone moja la damu. Akaingiza vibanzi chini ya makucha yake ya vidole, akisema kwa sauti kuu, “Allah, Allah, Allah! Allah, Allah, Allah! Allah, Allah,” namna hiyo. Mwislamu, na anadharau mawazo ya Yesu Kristo. Hakuwa na Roho Mtakatifu. La, la, bali alikuwa na mhemuko. Hiyo ni kweli. Sisi ni. . .

¹⁷² Ukristo hasa sana si mhemuko. Ukafiri unaweza kutoa saikolojia nyingi kama—kama—kama tu Ukristo uwezavyo; bali huo si Ukweli. Tunataka Kweli. Kristo ni Kweli.

¹⁷³ Tunafanya nini? Tulijifunga wenyewe hivi kwamba tunasimama kama Samsoni, sasa, wakati aliposimama pale akitafakari kile ambacho angalikuwa. Nafikiri, leo hii, kanisa linapaswa kusimama na kutafakari pamoja nami, dakika chache, kile tungalikuwa kama vitu hivi havingekuwa vimefanya hivi. Kile tungalikuwa!

¹⁷⁴ Ndipo likaja niani mwake, jambo fulani likaja. Ninaamini Mungu alilileta. Loo, laiti ingalitukia kwenye uwanja huu! “Kuna uwezekano.” Kuna uwezekano. Mungu anasamehe. Kuna uwezekano.

¹⁷⁵ Hatuna muda mrefu wa kukaa hapa. Muda wetu unaisha. Baraza la makanisa linaichukua nchi. Litaungana na Ukatoliki. Tuna mtu hapo ndani vile vile hasa.

¹⁷⁶ Laiti ningalikuwa na wakati wa kuliendea, kuwaonyesha ya kwamba taifa hili liko kama Israeli hasa. Walikuja kwenye nchi ya kigeni, wakawafukuza wenyeji, kisha wakairithi nchi. Hivyo ndivyo tulivyofanya. Israeli, walikuwa na mtu wa kwanza, mtu mashuhuri, mtu kama YOSHUA, mtu kama DAUDI, kama SULEMANI; bali hatimaye akaja mtu kwenye—kwenye ufalme, Ahabu fulani, haini. Tulikuwa na watu mashuhuri, Washington, Lincoln; bali sasa wamefanya nini? Kitu kile kile kilichotufanya tuje hapa kwa ajili ya uhuru wake, mmekiweka kwenye Ikulu, kwa sababu mnawazia zaidi juu ya siasa zenu kuliko mnavyowaza kumhusu Kristo. Kweli kabisa.

¹⁷⁷ Basi kumbukeni, katika wakati huo, wahudumu wote walijisalimisha. Yezebeli alikuwa ndiye kiongozi. Sikilizeni, Ahabu mwenyewe alikuwa ni jamaa mzuri kweli, bali Yezebeli alikuwa ndiye shingo nyuma ya kichwa. Ndiye aliyefanya hivyo. Alikuwa ndiye haini. Sina kitu dhidi ya mtu huyo, kama rais, bali ni huo mfumo wa Yezebeli ulio nyuma yake. Hivi hamwezi kuliona, hawa mapapa na kadhalika wanaokuja sasa, mmoja anainuka “asiyemjua Yusufu.” Ndipo muda si muda wajua, sasa hivi tunaliomba kanisa la Protestanti kuungana nalo, na kila dhehebu litaingia moja kwa moja katika baraza la makanisa, na hapo mmenaswa.

¹⁷⁸ Tunaishi kwa fedha za kodi ambazo zitalipwa katika muda wa miaka arobaini kuanzia leo. Taifa hili limefilisika. Ziko wapi? Ni nani aliye na fedha? Sisi hatuna? Hati ze—zetu hazifai kitu. Hatuna budi kuwa na dhahabu. Ni nani aliye nazo? Kanisa Katoliki. Watafanya nini? Kabla huyu mtu wa wiski na hawa wenye mali wakuu na wote wenye hisa hawajaziachilia, wataziua zote kabisa, nalo kanisa litalikopesha taifa fedha. Na litakavyofanya, litauza haki zake za mzaliwa wa kwanza moja kwa moja katika Ukatoliki. Basi mtafanya nini? Hiyo ndiyo

dhahabu ya ulimwengu, hao pamoja na Wayahudi, na hilo ndilo lile agano analofanya na Israeli.

¹⁷⁹ Mnaona, ninyi wasomaji wa Biblia mnaweza kufundisha hilo kanisani mwenu. Mnaona, ninawaonyesha tu ninaamini jambo lilo hilo.

¹⁸⁰ Hivyo ndivyo italibidi litimie, nasi tunalo pale pale sasa. Na sisi hapa, dhehebu, huku alama ya mnyama ikiwa juu yetu, kama tu yule mnyama wa kwanza; sanamu yake, baraza la makanisa, likijiunga na nguvu fulani. Nao wakafanya sanamu ya mnyama, naye angeweza kunena, naye anafanya jambo lile lile yule mnyama wa kwanza alilofanya mbele yake. Moja kwa moja mikononi mwetu! Loo, enyi watoto!

¹⁸¹ Ni wakati gani? “Je! kuna uwezekano?” Samsoni alisimama pale na kusema. Wakati gani? Ninii tu, “Je! kuna uwezekano?” Ilitokea Samsoni aliwazia, “Yule Mungu mkuu! Yeye yuko kila mahali. Yeye ni Mungu wa milele. Ninaliona kosa langu. Nitatubu.” Naye akalia kwa sauti kuu.

¹⁸² Kuna uwezekano kwamba tungeweza kufanya jambo lile lile. Hao wa siku hiyo. . . Siku hizi hawaoni ono, kama Samsoni. Laiti tungalionga tu ono la uwezekano! Anzia papa hapa, sasa hivi. Uwezekano, mnaona.

¹⁸³ Wanaketi kimya, na kupiga makofi, na kushangaa kile kitakachokuwa hatimaye. Mtaona siku moja, mtatokea kwenye ule mwisho mdogo wa pembe, mnaona, wakati huo. Mna makusanyiko makubwa, na yanametameta, mambo ya ulimwengu, “Loo, tunafikiri, vema, mnajua nini? Tuna wafuasi wengi kuliko tuliowahi kuwa nao. Nasi tunaweza kujenga mijengo ya mabilioni ya dola, tuna pesa nyingi kuliko tulizowahi kuwa nazo, makanisa bora labda kuliko baadhi ya Waprotestanti ama baadhi ya hao wengine waliyo nayo. Loo, jamani! Masomo; vema, tunawapeleka watoto wetu shuleni, na kuwajengea seminari mpya ili waingie.”

¹⁸⁴ Hebu niwaambieni sasa hivi. Mtu mwenye elimu, bila Roho Mtakatifu, anajipeleka mwenyewe, kwa kila digrii anayopata, mbali zaidi na Mungu. Hiyo ni kweli. Unasema, “Nina Digrii ya Sanaa.” Basi uko mbali zaidi kidogo kuliko ulivyokuwa. Wanapasua yai katika atomi, na kujikwaa juu ya jani la unyasi ambalo hawajui chochote kulihusu. Mmesikia ule msemu wa kale, “Wapumbavu watatembea kwa viatu vya njumu, ambapo Malaika wanaogopa kukanyaga.” Hiyo ni kweli, masomo, bali hayamleti Roho. Hayaleti matendo na Uzima wa Yesu Kristo.

¹⁸⁵ Shida yake ni kwamba, kanisa leo hii sio kama Samsoni. Hawako tayari kulipa gharama. Samsoni aliomba vema hapo alipoomba, “Bwana, jalia nife pamoja na adui.” Alijua ilikuwa inaenda kumgharimu kitu fulani. Alijua ilikuwa inaenda kugharimu kitu fulani. Inaenda kukugharimu kitu fulani, inaenda kunigharimu kitu fulani; hadhi yako ya jamii, nafasi

yako na wadhifa katika dhehebu. “Bwana, jalia nife, basi. Ninaona kusudi Lako.” Alijua ilikuwa inaenda kumgharimu kitu fulani. Lazima uwe tayari kufa, kwa adui wako, upate kuingia katika baraka za Mungu. Samsoni alikuwa tayari kulipa gharama, kusudi apate nguvu za Mungu tena juu yake. Alikuwa tayari kufanya hivyo. Je! uko tayari?

¹⁸⁶ Uko tayari kusalimisha vipindi vyako vya televisheni? Na, mnajua, ilikuwa ni makosa kwetu kwenda kuona sinema. Lakini sasa ibilisi amewashinda akili, akaiingiza moja kwa moja nyumbani pamoja na nyinyi. Hiyo ni kweli. Mnaona?

¹⁸⁷ Nilizoea kushuka kwenda kwa mzee mhubiri wa Kimethodisti, alizoea kuimba wimbo:

Tulishusha chini uzio, tulishusha chini uzio,
Tukapatana na dhambi.
Tulishusha chini uzio, kondoo wakatoka
Lakini nao mbuzi waliingiaje?

Mlishusha chini uzio, hivyo tu.

¹⁸⁸ Loo, ninamsikia mtu fulani akisema, “Sasa ngoja kidogo, Ndugu Branham, tunayo miamsho!” Naam, ni kitu gani? Uamsho wa kidhehebu. Hiyo ni kweli. Angalieni uadilifu wenu na tofauti zenu. Ni uamsho? Kuna wakati wa kutengana? Kuna wakati ambapo kila mtu anaweza kushirikiana pamoja na kupata ushirika? Kama dhehebu lako liko ndani yake, “ni sawa.” Kuenda mbali na Neno wakati wote, hiyo ni kweli, kuwafanya maaskofu wapya na kila kitu. Mnaona?

¹⁸⁹ Samsoni alijua ya kwamba hali yake ya sasa ya kurudi nyuma isingeweza kutoa nguvu za changamoto ya wakati huo.

¹⁹⁰ Wanaume na wanawake, ndugu zangu na dada, hebu niseme hili. Kanisa, katika hali yake ya sasa ya kimadhehebu, haliwezi kutoa nguvu kukabiliana na wakati huu, kuuita wakati. Wanaume na wanawake wanamtaka Mungu, mioyo miaminifu. Nawe unaweza kuwaacha wa—wa umoja na uende kwa wa uwili, huenda ukawaacha wa uwili ukaenda kwa wa utatu, na huenda ukafanya yote *haya, yale*, ama *mengineyo*; unavuta tu karatasi, ama—ama kuhamia-hamia kwenye misheni, ama kutenda kama sijui nini, mtoto wa kitoto. Hiyo ni kweli. Hulipati jinsi hiyo. Nguvu zetu za kurudi nyuma, haziwezi kukabiliana na changamoto ya wakati huu. Madhehebu hayatachukua thibitisho la Neno.

¹⁹¹ Wakati, Yesu Kristo, kama nilivyojaribu kuwaambia jana usiku, aliahidi hili katika siku za mwisho. Aliahidi kuwa nalo hapa. Nanyi mnajua hilo, kwa Biblia. Na kwa miaka kumi na mitano, huku na huku kote katika taifa, nao wanazidi kuwa wabaya zaidi wakati wote. Hiyo ni kweli. Mnaona, hawalitaki.

¹⁹² Wao wanasema, “Vema, sasa, yeye hushirikiana na wa umoja,” ama, “Yeye hushirikiana na wa utatu. Hufanya *hivi, vile*,

ama *vinginevyo*.” Tunashirikiana na Kristo, huko nje katika kila dhehebu, tukijaribu . . .

¹⁹³ Lakini Mungu huhakikisha hilo, kwamba wanaliona Hilo. Nao waaminio halisi ni kama maskini yule kahaba, jana usiku; mara Hiyo ilipomulika njiani mwake, na hiyo mbegu ya Uzima imekaa pale, yeye akaliamini Hilo. Hakuna lingine, iliwasha moto sasa hivi. Wakati kulikuwako na maelfu wamesimama pale, wakiidhihaki Hiyo, bali si yeye. Yeye alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ni ahadi, kwamba, wakati Yeye atakapokuja, Yeye angefanya hivyo.

¹⁹⁴ Nashangaa, laiti tu tungalijua jambo lile lile! Hivi tumefungwa sana na dhehebu letu, hata tumekatazwa kuliangalia Hilo? Nashangaa kama unayaangalia ma—magazeti na picha, na maskini mambo machafu ya kinyaa cha ulimwengu, badala ya kuisoma Biblia yako kama unavyopaswa kufanya? “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

¹⁹⁵ Watoto wetu, wavulana wetu, wamekuwa kundi la maskini akina Riki na Riketa, mnajua hiyo ni kweli, kundi la waliozama katika anasa na kila kitu namna hiyo. Nawe unampata wapi mvulana wa Kipentekoste? Akiendesha gari lake la kasi, mtaani. Unampata wapi dada? Huko chini kwenye kantini mahali fulani, akicheza roki? Unawapata wapi baba na mama? Baba, nje akicheza gofu, ama huko nje mahali fulani namna hiyo, naye mama nje kwenye karamu ya kushona ya chama fulani alichu mwanachama, ama kitu fulani. Wakati, inapaswa kuwa ni nyumba iliyokusanyika pamoja chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, huku Biblia imerudi tena. Huko ndiko tumechukuliwa tukafikia. Sio kukosoa, bali kuwatikisa tu kidogo, mnaona, ili mwelewe.

¹⁹⁶ Wakati wote, na (loo, sina budi kufunga) Wafilisti kamwe hawakuona kile kilichokuwa kikiendelea. Kuna kitu kilichokuwa kikiendelea, maana kitu fulani kilianza kusogea moyoni mwa Samsoni, “Kulikuwa na uwezekano,” mnaona. Akaigusa aone kama ilikuwa ingali pale.

¹⁹⁷ Wanawake wengine wana wakati mgumu sasa, wakijua ilipaswa kuwa nayo. Lakini aone kama ahadi Yake ingaliko, aone kama Yeye angali alifanya . . . Gusa tu nyuma uone kama Yeye si yule yule jana, leo, na hata milele.

¹⁹⁸ Akaigusa. Alijua kulikuwako na kitu. Akainua kichwa chake. Hakuwa na macho. Hawakuyaona machozi yakitirika kutoka kwenye hayo matundu matupu, ambamo zile tezi zilikuwa zikiachilia machozi yatiririke. Kichwa chake juu, midomo yake ikisogea polepole, machozi yakitirika kutoka kwenye matundu hayo yaliyopofushwa. Alikuwa akitubu. Alijua ya kwamba Yehova angali aliishi. Ingawa alikuwa amekosea, alijua Yeye alikuwa angali ni Mungu. Machozi

yakitiririka kutoka mashavuni mwake, wakati akisimama pale. Wale Wafilisiti walikuwa wamelewa kupita kiasi hata wasingeona hilo.

¹⁹⁹ Kama wafuasi wako wa kanisa, wenzako kanisani hawaoni hilo, wewe endelea tu kuomba. Alitaka kuona, mara moja zaidi, Neno la Mungu likidhihirishwa mbele ya hilo kundi la makafiri walevi, waliopofuka, wasioamini. Kama hiyo ndiyo njaa ya kanisa leo hii, kuona mara moja zaidi, uamsho wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu, kutoka mimbarani moja kwa moja hata kwa bawabu, kusafishwa kwa mtindo wa kale, uamsho wa mtindo wa kale pamoja na nguvu za Mungu, I—Injili inayosafisha mtu kwelikweli, kutoka ndani mpaka nje; ya mtindo wa kale, ulionyoka kama mtutu wa bunduki, dini ya nyuma ya misitu, mbingu za samawati, inayoangamiza dhambi ambayo huondolea mbali Hollywood yote kutoka kwako, hao wanaopendelea.

²⁰⁰ Huyu hapo, akiomba. Sio dhehebu jipya sasa, kanuni mpya ya imani; bali thibitisho la Neno. “Bwana, Wewe ulikuwa juu yangu wakati mmoja, Wewe ulinipa nguvu wakati mmoja. Laiti ningalikuwa tu na hizo nguvu! Ninayo misuli, bali ni dhaifu.”

²⁰¹ Tunao washiriki, bali ni dhaifu. Wanayapenda mambo ya ulimwengu kuliko wanavyoyapenda mambo... Unasema mimi sana sana ni... Loo? Hebu yaangalie makanisa upate kujua. Usijaribu kulikana. Matendo yako yanazungumza kuliko maneno yako yafanyavyo, unaona. Loo, naam, tuna wafuasi zaidi, misuli mikubwa zaidi, lakini ziko wapi nguvu za Bwana? Misuli yako mikubwa haitakabiliana na changamoto ya wakati huu, ile imani ya kunyakuliwa kulitwaa Kanisa kutoka kwenye kitu hiki kabla hukumu haijaipiga dunia.

²⁰² Nayo hukumu iko karibu kupiga. Nitasema, kama vile rafiki yangu Jack Moore alivyosema; kama Mungu akiachilia Marekani isiwajibike kwa mambo inayofanya sasa, Yeye atawajibika kimaadili kuifufufa Sodoma na Gomora na kuiomba msamaha, kwa ajili ya kuiteketeza. Kweli! Hukumu inafuata.

²⁰³ Mungu, ondoa ulimwengu wote kutoka kwangu. Nipe imani, Ee Bwana, kwa ajili ya Unyakuo. Kwa kuwa, kutakuwako na wawili kitandani, na mmoja atachukuliwa, mmoja aachwe. Wawili watakuwa kwenye—kwenye kiti cha motokaa, na mmoja atachukuliwa na mmoja ataachwa. Itatukia katika dakika moja.

Unasema, “Ndugu Branham, itakuwa lini?”

²⁰⁴ Huenda ukakosoa hili. (Kama ni sawa kulisema?) [Wahudumu wanasema, “Endelea ukaliseme, ndugu.”—Mh.] Hebu niangushe kitu kidogo hapa. Siku moja mtagundua.

²⁰⁵ Mtasema kule, “Loo, nimefundishwa ya kwamba kuna *hili*, *lile*, na *lile lingine*, linaloenda kutukia kabla Bwana

hajaja. Kutakuwako na kipindi cha dhiki kuu, nasi tutakipitia.” Mnaona? Mnaona?

206 Mnajua, wakati mmoja Yesu aliulizwa swali. Akasema, “Ni kwa nini waandishi wanasema ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?”

207 Naye Yesu akasema, “Nawaambia, Yeye amekuja tayari, wala hamkujua.”

208 Moja ya siku hizi mtasema, “Vema, nilifikiri Kanisa lilikuwa linaenda, lilipaswa kufanya *hivi, vile*, na *vinginevyo*. Nilidhani kungekuwako na Unyakuo. Nilidhani. . .”

209 Mnaona, itakuwa ni kunyakuliwa kwa siri. Kama alimchukua mmoja hapa Hot Springs, na mmoja mahali pengine, na mmoja kule chini, na mmoja kule, itajumuisha hasa mamilioni ya hao watakaotoka ardhini. Na kuna angalau watu mia tano, kila siku, wanaokosekana ulimwenguni, wala hata hatujui mahali walikoenda. Mnaona, Unyakuo utawajumuisha wale wote waliolala mavumbini mwa nchi, walio sawa na Mungu.

Watasema, “Vema, nilidhani Unyakuo ulikuwa utukie.”

“Umepita tayari, wala hukujua. Umeachwa.” Unaona?

“Vema, kila kitu kinaenda. . .” Naam, bwana.

210 Ni Kuja kwa siri, ndivyo Unyakuo ulivyo, anakuja kuiba. Kama kile kitabu nilichosoma wakati ule (kiliitwaje), Juliet na Romeo. Alikuwa usiku, wakati watu walikuwa wamelala katika mambo ya ulimwengu, na kanisa lote katika mambo ya ulimwengu. Ndipo mara ghafla, mlilo ukaja, nao hao wakaondoka.

211 Sikilizeni, mmesikia mengi sana katika Wafanyabiashara Wakristo, Watu wa Full Gospel, wakisema, “Loo, mwajua, Kasisi Baba Mtakatifu *Nanii-wa-nanii*! Wapresbiteri wanaanza kupokea Roho Mtakatifu. Walutheri wanaanza kupokea Roho Mtakatifu.”

212 Enyi kundi la watu waliolala! Hivi hamjui? Yesu alisema, “Wakati huyo mwanamwali aliyelala atakapokuja kununua Mafuta, ilikuwa ni wakati uo huo ambapo Bwana-arusi alikuja, naye akaingia.” Kumbukeni, hawakuyapata Hayo! Je! hiyo ni kweli? Kama vile Booth-Clibborn alivyosema, “Ha?” A-ha. Huenda wao, walipitia mihemuko fulani, bali kweli hawakuyapata Hayo. Walipokuja kununua Mafuta, ilikuwa imechelewa sana.

213 Nao hawa hapa sasa, Mpresbiteri, Mlutheri; hebu angalia kwenye *Sauti* ya Wafanyabiashara wa Full Gospel, na hilo kundi la wajukuu wa Kipentekoste pamoja na ndugu hawa wa kimadhehebu, wakifikiri ya kwamba hilo ni jambo kuu. Huenda ukauliza siku moja, “Vema, nilidhania *hivi*.”

214 “Limepita tayari, nawe hukujua.” Hebu nisimame hapo, kwa sababu si—sipo hapa kuhubiri fundisho.

215 Lakini, uwezekano! Kamwe usibahatishe. Hii ndiyo siku. Hii ndiyo saa. Kuna uwezekano sasa hivi, labda si kwenye saa kumi na moja. Kuna uwezekano. “Bwana, ninajua Wewe ni Mungu. Ninajua Wewe ndiye. Niko mbali na Wewe. Lakini ninajua kwamba hii mishipa yangu wakati mmoja ilivuma na nguvu za Mungu. Ninajua mambo ninayojali leo hii, ninadai kuwa Mpentekoste;” wanawake, “Mimi hukata nywele zangu;” mwanamume, “Mimi hufanya *hivi, vile, ama vinginevyo*.”

216 Nanyi wanaume ambao mtawaruhusu wake zenu wavae kaptura na kufanya mambo hayo, halafu ujiite mwenyewe mwana wa Mungu, aibu kwako.

217 Nilienda kwenye kanisa fulani kubwa la kimadhehebu, sio muda mrefu uliopita, kwenye ninii... Walikuwa na mkutano, nami nikatoka kwenda kuwatembelea. Basi mchungaji alinipeleka huko nje, naye alikuwa anaenda kunitambulisha kwa mke wake. Alikuwa ndiye mpiga piano. Naye mwanamke huyo alikuwa na nguo iliyombana sana hata karibu ngozi ilikuwa nje. Alikuwa amejipaka vipodozi, na alivaa kila namna ya vitu masikioni mwake.

218 Ndipo nikasema, “Ndugu, unataka kusema kwamba mke wa—wako ni mtakatifu?”

Kasema, “Naam, bwana.”

219 Nikasema, “Anaonekana kama mtakataka.” Nikasema, “Sijawahi kuona kitu kama hicho katika jina la Pentekoste na utakatifu!”

220 Loo, ndugu, tunahitaji kusafishwa kwa nyumba, kuanzia mimbarani hadi chumba cha chini. Na moja ya siku hizi... Unasema, “Mimi ni Mpentekoste.” Hilo halimaanishi zaidi ya kuwa nguruwe, kwa Mungu. Hilo halina uhusiano wowote na Kristo. Hilo ni jina tu. Inakubidi kuwa Pentekoste moyoni mwako, matunda ya Roho. Angalieni. Loo, jamani!

221 Alijua kile kingetukia kama Mungu alijibu maombi yake.

222 Je! unajua? Unajua kwamba dhehebu litakufukuza? Unatambua ya kwamba sasa hivi unaingia moja kwa moja kwenye muungano wa makanisa, na vitu ambavyo mnaingia moja kwa moja ndani yake? Unatambua kile ambacho itakugharimu? Unajua hao wanawake unaocheza nao kamari watakuita “mtindo wa kale” na upuuzi wote wa namna hiyo? Maana hutawaruhusu watoto wako wavae kaptura, nawe unafanya mambo haya, unajua itakachokugharimu? Afadhali ufanye hesabu kabla hujaanza, unaona. Afadhali uliwazie. Naam. Afadhali—afadhali ushauriane na Mungu, kwanza, kabla hujaanza.

²²³ Alijua, kama maombi yake yangejibiwa; bali alikuwa tayari, na yeye alikuwa mwaminifu.

²²⁴ Laiti kanisa lingeweza tu kuingia katika hali hiyo! Kama uko tayari sasa hivi, kama wewe ni mwaminifu, kama kweli unamaanisha, kama macho yako yamefunguliwa kwa yale ninayotaribu kukwambia kwa njia mzunguko! Iwapo wewe ni mwaminifu, basi sema, “Bwana, sijali ni nini, niko tayari. Ninaiona ishara. Ninajua ya kwamba kumechelewa kuliko tunavyodhania. Ni wakati wa kuja.”

²²⁵ Ndipo Samsoni akasema kwa sauti kuu, “Bwana, waliyang’oa macho yangu. Ninajua ya kwamba Wewe ni Mungu. Ninajua ya kwamba Wewe una nguvu za kufanya hivyo. Ninajua Wewe unaweza kuniweka huru na pingu hizi. Mara moja tu zaidi, Bwana, mara moja tu zaidi!”

²²⁶ Mara moja tu zaidi, Bwana, mara moja tu zaidi! Hebu na kuwe na mkutano wa kambi kando ya kilima, kama kulivyokuwako kilimani kwenye Chumba cha Juu. Hebu na ije sauti kutoka Mbinguni, kama upepo mkali ukienda kasi, uijaze nyumba yote, ushuhuda unaonekana wa Kristo aliyeufuka.

²²⁷ “Mara moja tu zaidi, Bwana, mara moja tu zaidi,” akalia. Wakati alipolia, katika uaminifu, amesimama pale, huku macho yake yamepofushwa. “Ninajua gharama, Bwana, lakini mara moja tu zaidi!”

²²⁸ Mungu huyajibu maombi. Akahisi mishipa ikikaza. Misuli yake ikaanza kushikilia. Nguvu za mguu wake zikaanza kurudi. Akamwambia yule mvulana mdogo, “Niongoze kwenye nguzo sasa.”

²²⁹ “Niongoze, Bwana, niongoze. Niongoze kwenye ile nguzo, kwa Kalvari. Niongoze kwenye nguzo ambapo ninaweza kusulubiwa, mpaka maisha yangu ya kale ya kilimwengu yafie hapa nje, na yote niliyo mimi. Niongoze kwenye nguzo, Bwana.”

²³⁰ Wakati alipoanza kuihisi hiyo misuli ikikaza kwa nguvu za Mungu, haikumbidi kuona kilichokuwa kikitukia, yeye alihisi kilichokuwa kikitukia. Akaanza kuyanyonganyonga mabega yake, na, alipofanya hivyo, hilo jengo likaporomoka. Siku hiyo, alishinda, aliwaua Wafilisti wengi kuliko wale aliowaua siku zote za maisha yake.

²³¹ Enyi marafiki, kuna uwezekano ya kwamba kanisa hili, katika hali hii...Sasa nina yapata kurasa tatu ama nne za muhtasari pale, ninaenda kuachilia. Kuna uwezekano. Upo uwezekano papa hapa kwenye mkutano huu wa kambi. Kuna uwezekano papa hapa kwenye saa hii. Kuna uwezekano, kama tuko tayari kulipa gharama, tunaweza kuona Matendo 2 nyingine ikitukia.

²³² “Mara moja zaidi, Bwana! Tumelivuruga. Tumeunda dhehebu. Tumevunjilia mbali udugu wetu. Tumetenganisha

ushirika wetu. Tumechukua kundi dogo *huku*. Tunapigana vita mmoja na mwingine, naye ibilisi ameketi kitako, akituangalia tukicharazana. Bwana, inawezekana kwamba mara moja zaidi kwamba sisi sote mia na ishirini tunaweza kuwa katika moyo mmoja mahali pamoja? Inawezekana ije sauti kutoka Mbinguni, kama upepo mkali wenye nguvu ukienda kasi? Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!”

²³³ Na tusimame kwa miguu yetu, na kusema, “Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi, Bwana!”

²³⁴ Ee Bwana Mungu, nisikie, Bwana. Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi itume Roho juu ya mkutano huu wa kambi, katika nguvu na utukufu!



EE BWANA, MARA MOJA TU ZAIDI SWA63-0628M

(O Lord, Just Once More)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa asubuhi, tarehe 28 Juni, mwaka wa 1963, kwenye Uga wa Shirika la Udugu wa Wakristo huko Hot Springs, Arkansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org